

MATUMIZI YA USONDE NAFSI NA USONDE JAMII: MTAZAMO WA UHUSIANO

OKEYO JULIET SUSAN

C50/66361/2011

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA KISWAHILI

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

2013

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili wa sanaa katika chuo kikuu kingine chochote.

.....

Tarehe:

Okeyo Juliet Susan

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama washauri na wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.

.....

Tarehe:

Dkt. Iribi Mwangi

(Msimamizi)

.....

Tarehe:

Bw. Gitonga Josephat

(Msimamizi)

TABARUKU

Kwa mwanangu David Siwa (Jnr) na wazazi wangu David Siwa Okeyo (HSC, MBS), Rodah
Siwa Okeyo na Miriam Siwa

SHUKRANI

Natoa shukrani nyingi kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na uwezo wa kuyamudu masomo ya kiwango hiki. Bila yeze singefika katika kiwango hiki cha masomo. Neema, baraka na rehema zake zimenitosha.

Kazi hii imetimilika kwa sababu ya hisani na juhudini za watu mbalimbali. Kwanza ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt. Iribi Mwangi na Bw. Gitonga Josephat kwa kujitolea kusoma kila neno katika tasnifu hii. Nawashukuru kwa moyo wangu wote kwa ushauri mlionipa kila nilipohitaji ushauri wenu. Mbarikiwe.

Ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Kiswahili, Prof. Habwe, Prof. Kineene, Prof. Mbatia, Dkt. Zaja, Dkt. Mweri, Dkt. Mbuthia, Dkt. Swaleh na Bw. Mungania.

Natoa shukrani kwa wanafunzi wenzangu kwa mchango wao katika masomo yangu pamoja na kunipa moyo kila nilipokuwa nikikata tamaa. Wenzangu hawa ni pamoja na Otiende Meroline, Katutu Ruth, Nguti Mary, Owallah Kennedy, Muriithi Joshua, Ong'era G., Koech L., Moraal L., Kanywa G., Ludia F., Obiero R., Keter C., Ndumbu, Chacha, Muniu, Swakei, Njeri, Chepng'etich, Makange, Motuka na Angelina. Nawashukuru kwa urafiki wenu kwa miaka hii miwili ambayo tumekuwa katika darasa moja.

Namshukuru mwanangu David Siwa (Jnr) kwa kuwa mvumilivu kwa muda ambao sikuweza kutangamana naye kwa mambo mengi aliponihitaji. Namwombea aweze kutambua umuhimu wa masomo. Mungu akubariki.

Nawashukuru kwa moyo wa dhati wazazi wangu wapendwa David Siwa Okeyo (HSC, MBS), Rodah Siwa Okeyo na Miriam Siwa kwa kuniwekea msingi bora wa elimu, kunipa motisha katika masomo yangu pamoja na kuniombea dua njema wakati wa masomo yangu. Mungu awabariki.

Shukrani za kipekee nawatolea ndugu zangu Samson, Phillip, Alice, Emily na Joshua. Mungu awabariki kwa msaada mlionipa kila nilipowahitaji.

Nawashukuru rafiki zangu Mercy Oooke na Susan Rabah kwa maombi ya kunitakia mema kwenye masomo yangu pamoja na msaada walionipa.

UFAFANUZI WA ISTILAHI

USONDE

Usonde ni namna ambavyo ufasiri wa usemi hutegemea uchambuzi wa muktadha wa usemi kama vile anayezungumza, wakati na mahali pa kuzungumza.

USONDE NAFSI

Usonde nafsi hurejelea wahusika katika tukio la mawasiliano. Wahusika huwa msemaji ambaye huwa kiini cha usonde na msikilizaji (msemewa).

USONDE JAMII

Usonde jamii ni kule kuchunguza vipengele vya sentensi ambavyo huonyesha vigezo mbalimbali vya kijamii katika tendo usemi.

YALIYOMO

Jalada.....	i
Ungamo.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Ufafanuzi wa istilahi.....	vi
Yaliyomo.....	vii
Jedwali.....	x
Michoro.....	xi
Vifupisho vya Maneno.....	xii
Muhtasari.....	xiii
SURA YA KWANZA.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	2
1.3 Malengo ya Utafiti.....	2
1.4 Nadharia Tete.....	2
1.5 Sababu ya Kuchagua Mada.....	3
1.6 Upeo na Mipaka.....	3
1.7 Msingi wa Nadharia.....	4
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii.....	10
1.9 Njia za Utafiti.....	11
1.9.1 Aina ya Utafiti.....	12
1.9.2 Data na Njia za Kukusanya Data.....	12
1.9.3 Idadi ya Watafitiwa na Sampuli.....	13
1.9.4 Njia za Kuchambua Data.....	13
1.10 Muhtasari wa Sura.....	14

SURA YA PILI: VIPENGELE MUHIMU KATIKA USONDE.....	15
2.1 Utangulizi.....	15
2.2 Dhana ya Usonde.....	15
2.3 Kiini cha Usonde.....	16
2.4 Matumizi ya Usonde.....	19
2.5 Anafora.....	20
2.6 Muktadha.....	21
2.7 Matamko.....	22
2.8 Hitimisho.....	24
SURA YA TATU: USONDE NAFSI NA USONDE JAMII KATIKA KISWAHILI.....	26
3.1 Utangulizi.....	26
3.2 Usonde Nafsi.....	26
3.2.1 Viwakilishi vya Nafsi.....	26
3.2.1.1 Nafsi ya Kwanza.....	28
3.2.1.2 Nafsi ya Pili.....	31
3.2.1.2.1 Kauli za Mnени.....	33
3.2.1.3 Nafsi ya Tatuu.....	34
3.2.2 Viwakilishi Vimilikishi.....	36
3.2.3 Viwakilishi Virejeshi.....	38
3.3 Usonde Jamii.....	40
3.4 Hitimisho.....	45
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA.....	46
4.1 Utangulizi.....	46
4.2 Usonde Nafsi.....	46
4.2.1 Nafsi ya Kwanza.....	46
4.2.2 Nafsi ya Pili.....	51
4.2.2.1 Kauli za Mneni.....	53

4.2.3	Nafsi ya Tatu.....	54
4.2.4	Vimilikishi.....	55
4.3	Usonde Jamii.....	57
4.4	Majadiliano.....	60
4.5	Hitimisho.....	61
SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....		62
5.1	Utangulizi.....	62
5.2	Hitimisho.....	62
5.3	Mapendekezo.....	63
MAREJELEO.....		64
KIAMBATANISHO		

JEDWALI

Jedwali la Vionyeshi.....	17
Jedwali la Viwakilishi vya Nafsi.....	27
Jedwali la Nafsi na Vimilikishi.....	36
Jedwali la Ngeli, Nafsi na Vimilikishi.....	37
Jedwali la Ngeli na Viwakilishi Virejeshi.....	39
Jedwali la Vigezo vya Heshima.....	41

MICHORO

Mchoro wa Uhusika Katika Tukio la Mawasiliano.....	27
Mchoro wa Kushirikisha Msemewa.....	29
Mchoro wa Kutoshirikisha Msemewa.....	30
Mchoro wa Kutoshirikisha Msemaji.....	31
Mchoro wa “Mwingine” Katika Nafsi ya Pili Wingi.....	32
Mchoro wa Nafsi ya Tatu.....	34

VIFUPISHO VYA MANENO

nk - Na Kadhalika

kv - Kama Vile

taz - Tazama

uk - Ukurasa

MUHTASARI

Utafiti huu umeshughulikia matumizi ya usonde nafsi na usonde jamii katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili. Tumetumia nadharia ya uhusiano kwa sababu ya sifa ya usonde ya kutegemea muktadha kwenye ufasiri wa maneno yake. Vivyo hivyo tumechagua kutafitia usonde nafsi na usonde jamii ili kutathmini wazo la Marmaridou (2000) kuwa kategoria hizi mbili za usonde zina mtagusano kiasi cha kuchukuliwa kuwa ni kategoria moja.

Utafiti huu ulifanywa kwa kutumia utafiti stahilifu kimaelezo kwa kuwa data ambayo ilikusanya ilikuwa katika umbo la maneno tamkwa ya walimu na wanafunzi. Hatua zilizotumiwa katika ukusanyaji ni pamoja na kusikiliza, kurekodi na kuandika. Data ilichanganuliwa kwa kutumia utaratibu wa kusimba pronomino pamoja na hatua za uzulishaji katika utaratibu wa ufahamu katika nadharia ya uhusiano.

Hatimaye utafiti huu umeshikilia kuwa, katika lugha ya Kiswahili kuna uhusiano kati ya usonde nafsi na usonde jamii hasa katika baadhi ya matumizi ya usonde nafsi. Kwa hivyo haipaswi kushikilia kuwa usonde nafsi na usonde jamii ni kategoria moja ya usonde.

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi

Mawasiliano ambayo ni muhimu sana katika maisha ya binadamu huwa ama ya kimaandishi, kimatamshi au kiishara. Katika mawasiliano yoyote lazima kuwe na mzungumzaji na msikilizaji ambao huwa na mahusiano mbalimbali ya kijamii kama vile mahusiano ya wazazi na wanao, kirafiki, kikazi, kidini na mengineo. Mahusiano haya huweza kuathiri namna ambavyo watu huwasiliana.

Kulingana na Levinson (1983) usonde ni namna ambavyo ufasiri wa usemi hutegemea uchambuzi wa muktadha wa usemi kama vile anayezungumza, wakati na mahali pa kuzungumza. Levinson alidondoa aina tano za usonde: jamii, nafsi, wakati, makala na mahali. Fillmore (1971) ameieleza dhana ya usonde kuwa ni istilahi ambayo hurejelea matumizi ya vipengee au kategoria za maneno na sarufi ambayo hudhibitiwa na mambo fulani katika muktadha wa mazungumzo. Yule (1996) alifafanua usonde kama maneno ya kuashiria.

Dhana ya usonde hutumika katika semantiki kuakisi uhusiano wa kurejelea muktadha ambamo msemaji na msikilizaji huwa. Maneno yanayotumiwa katika urejelezi wa kiusonde mara nyingi huwa hayana maana inayolengwa; maana hujitokeza kwa kile kinachoashiriwa (Habwe na Karanja, 2004).

Matamshi kama mimi, wewe, sisi, kule, hapa, jana na leo yanahusishwa na msemaji katika uzungumzaji; yaani maneno haya huchukua ufasiri wao kutoka kwenye msemaji wakati wa usemi. Kwa hivyo ni muhimu kwa msikilizaji kumtambua msemaji, wakati wa usemi na mahali pa usemi ili aweze kufasiri kilichosemwa na umaanisho katika usemi huo.

Matumizi ya usonde nafsi na usonde jamii yakishirikishwa na nadharia ya uhusiano (nadharia ambayo inahusu ufasiri wa maana za matamko) yametutia changamoto ya kuyatafitia kwa sababu ni sehemu ya mazungumzo yetu ya kila siku ambayo ni pamoja na mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi wao.

1.2 Tatizo la Utafiti

Marmaridou (2000) anaeleza kuwa usonde nafsi na usonde jamii ni kategoria moja ya usonde. Kulingana na Marmaridou kuainisha makundi haya mawili ya usonde kunatatiza kwa kuwa huwezi kuwa na usonde nafsi pekee bila ya kuihusisha na usonde jamii. Pengo hili ndilo ambalo utafiti huu unanuia kuliziba kwa kuchunguza namna ambavyo makundi haya mawili ya usonde yanavyoingiliana. Kwa kuliziba pengo hili utafiti huu utajibu maswali kama: Je, mazungumzo ya walimu na wanafunzi katika lugha ya Kiswahili hubainisha matumizi ya makundi haya mawili ya usonde? Je, uhusiano uliopo baina ya usonde jamii na usonde nafsi inatosheleza kuweka aina hizi mbili za usonde katika kategoria moja?

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

- a) Kubainisha matumizi ya usonde nafsi katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.
- b) Kubainisha matumizi ya usonde jamii katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.
- c) Kuchunguza uhusiano uliopo kati ya usonde nafsi na usonde jamii.
- d) Kuchunguza ikiwa nadharia ya uhusiano inatosheleza kuchanganua maneno ya usonde jamii na usonde nafsi.

1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- a) Usonde nafsi haitumiwi katika mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.

- b) Usonde jamii haitumiwi katika mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.
- c) Kuna uhusiano kati ya usonde nafsi na usonde jamii.
- d) Nadharia ya uhusiano inatosheleza kuchanganua maneno ya usonde jamii na usonde nafsi.

1.5 Sababu ya Kuchagua Mada

Tuliichagua mada hii ili kuthibitisha iwapo kuna uhusiano baina ya usonde jamii na usonde nafsi kulingana na mtazamo wa Marmaridou (2000).

Sababu ingine ya kuchagua mada hii ni kutokana na msimamo wa Levinson (1983) kuwa kategoria za usonde kama vile usonde nafsi ni kategoria biya za kisarufi ambazo zina majukumu muhimu katika ufunzaji wa lugha. Kategoria hizi hufafanuliwa kwa njia tofauti katika lugha za dunia. Kwa mfano lugha moja huweza kuwa na istilahi za kutajia nafsi ya tatu na nyingine ikakosa istilahi hizo vivyo hivyo lugha kama Kiswahili haina istilahi za kutajia jinsia tofauti na lugha ya Kiingereza. Hivyo basi utafiti wetu utabainisha namna ambavyo maneno ya usonde hujitokeza katika lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu ulichoche na ari ya kutaka kujua mikakati ya ufasiri wa ujumbe katika lugha ya Kiswahili inavyoshirikishwa na walimu na wanafunzi wao katika mazungumzo yao.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulijikita katika nadharia ya uhusiano ya Sperber na Wilson (1986/1995 na 1993) kwa kuchunguza namna ambavyo maneno ya usonde huweza kufasiriwa kwenye mawasiliano ya walimu na wanafunzi katika lugha ya Kiswahili.

Kulingana na Levinson (1983) na Fillmore (1971, 1975) kimapokeo kunazo kategoria tano kuu za usonde. Hata hivyo utafiti huu ulijikita kwa matumizi ya usonde nafsi na usonde jamii katika

mazungumzo baina ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika Shule ya Upili ya Xaverian, Kisumu.

1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu ulijikita katika nadharia ya uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1986/1995 na 1993) na ambayo inahusu namna ambavyo msikilizaji hufasiri maana za matamko ya msemaji.

Nadharia hii huchukuliwa kuwa ni jaribio la kufafanua kwa kina mojawapo ya madai ya Grice (1989) kuwa kitu muhimu sana katika mawasiliano ya binadamu ni usemi na ufahamu wa kusudi la mawasiliano.

Sperber na Wilson wanashikilia kuwa kuna tofauti mbili kuu katika matumizi ya lugha: matumizi ya kimaelezo ambayo ni matumizi yanayotegemea ukweli na matumizi ya kiufasiri ambayo ni matumizi ya ufananisho. Kwa hivyo matamko hutumiwa kiufasiri ili kuwakilisha mawazo ya msemaji. Yaani matamko ni semi za kiufasiri za mawazo ambayo msemaji anataka kuwasilisha.

Kwa ujumla mawasiliano huwa na kiashiria hivi kwamba msemaji hunasa makini ya msemewa kupitia kiashiria hicho ambacho kitamuza msemewa kuwa msemaji ana jambo la kuwasilisha. Sperber na Wilson walikiita kiashiria hicho kiashiria wazi. Kwa hivyo mawasiliano yenye kiashiria wazi huitwa mawasiliano wazi.

Kulingana na nadharia hii mawasiliano wazi, kwa kawaida, huwa dayalojia yenye lengo mawasiliano na lengo ujumbe. Lengo ujumbe ni nia ya msemaji kumjuza msikilizaji kuhusu kitu fulani huku lengo mawasiliano likiwa ni lengo la msemaji kumjuza msikilizaji wake kuhusu lengo ujumbe (Sperber na Wilson, 1995).

Sperber na Wilson walipendekeza kanuni mbili za uhusiano: kanuni fahamu na kanuni mawasiliano.

Kanuni fahamu inashikilia kuwa ufahamu wa binadamu huegemea upevushaji wa uhusiano (1995: 260). Upevushaji huu hulenga kutimiza athari mbalimbali za kimuktadha kwa kutumia jitihada ndogo kabisa katika mchakato wa habari. Hivi ni kusema kuwa ili mawasiliano yafanikishwe msemaji huhitaji makini ya msikilizaji kwa hivyo lazima msemaji huyo ayafanye matamko yake kuwa ya uhusika iwezekanavyo ili kustahili makini ya msikilizaji.

Kwenye kanuni mawasiliano kila tendo katika mawasiliano wazi huwasilisha udhaniaji wa hali bora kabisa ya uhusiano (Sperber na Wilson, 1986:158). Yaani kiashiria wazi huwa na uhusiano bora kabisa pasi na jambo lolote lingine. Sperber na Wilson wamefafanua udhaniaji wa hali bora kabisa ya uhusiano ifuatavyo:

- (a) Kiashiria wazi kina uhusiano tosha ili kustahili jitihada ya msikilizaji kukifanyia mchakato.
- (b) Kiashiria wazi kiwe kile chenye uhusiano unaofaa zaidi na kiwe ambacho kinalingana na uwezo pamoja na mapendeleo ya mwasilishaji.

Kulingana na kanuni hizi msikilizaji ambaye amepokea kiashiria wazi cha msemaji, anatarajia udhaniaji wa hali bora zaidi ya uhusiano. Msikilizaji kwa hivyo huanza kuzua ujumbe ili apate ufasiri wa uhusiano pevu.

Sperber na Wilson wanaeleza kuwa uhusiano huweza kutathminiwa kwa kuangalia athari za kifahamu na athari za jitihada. Uhusiano pevu huwa na athari za kiwango cha juu za kifahamu lakini jitihada za mchakato huwa katika kiwango cha chini.

Athari za kifahamu, kulingana na nadharia hii, hutokana na badiliko la mazingira ya kifahamu. Badiliko hili husababishwa na muingiliano wa ujumbe mpya na mawazo yaliyomo akilini. Mazingira ya kifahamu yanayofanana ni muhimu kijamii kwa sababu bila mazingira haya shughuli kama vile uendeshaji wa magari hayawezekani. Kunazo aina tatu za badiliko hili la mazingira ya kifahamu kama ifuatavyo:

Kwanza maana kimuktadha huweza kuongezewa kwenye mazingira ya kifahamu. Maana hii ya kimuktadha ni uamuzi unaotokana na ujumbe mpya. Kwa mfano:

(1) Amina: Je, unapenda paka?

Maria: Sipendi wanyama.

i. Paka ni mnyama.

ii. Maria hapendi paka.

Ili kuelewa tamko la Maria, Amina anaweza kuwa na uchukulizi kuwa paka ni wanyama hali ambayo ilikuwemo kwenye mazingira yake ya kifahamu. Hapa tunaweza kusema kuwa mazingira ya kifahamu ya Amina yamebadilishwa na kule kuongezwa kwa maana kimuktadha.

Pili, mawazo yaliyomo huimarishwa kwa kutoa ushahidi zaidi. Kwa mfano:

(2) i. Ikiwa Maria anaogopa paka, Maria hawapendi paka.

ii. Maria anaogopa paka.

Kauli hizi zimeongezwa katika mfano (1) kama ujumbe mpya. Amina kwa hivyo anaweza kufikia uamuzi kutokana na (2i) na (2ii). Maria kutopenda wanyama ni wazo lililokuwemo wala si maana kimuktadha, kwa hivyo “Maria kutopenda wanyama” inaimarishwa na ujumbe mpya ambao ni (2).

Tatu ni ukinzani na uondoshaji wa mawazo yaliyomo na ambayo yanaonekana kama yasiyo ya kweli. Yaani, ikiwa ujumbe mpya na mawazo yaliyomo yanakinzana, ile hafifu kati yao huondolewa. Kwa mfano:

(3) i. Kama Maria ana paka, Maria anapenda paka,

ii. Maria ana paka.

iii. Maria anapenda paka.

Mfano (3) umeongezwa kwa (1) kama ujumbe mpya. Amina anaweza kufikia maana kimuktadha (3iii) kutoka kwa (3i) na (3ii) lakini (3iii) inakinzana na (1ii). Ikiwa (1ii) ni hafifu kuliko (3iii) basi itaondoshwa na ikiwa (3iii) ni hafifu kuliko (1ii), (3iii) itaondoshwa.

Sperber na Wilson wanasema kuwa kunazo njia tatu kuu za kubainisha jitihada za mchakato kama ifuatavyo:

Uchangamano wa tamko: Ikiwa uchangamano wa tamko ni wa kiasi cha juu basi jitihada za mchakato zitakuwa nyingi zaidi.

Kipimo cha muktadha: Kipimo cha muktadha kikiwa kikubwa sana, jitihada za mchakato zitakuwa nyingi zaidi.

Upatikanaji wa muktadha: Upatikanaji ukiwa katika kiwango cha chini kabisa basi jitihada za mchakato zitakuwa nyingi zaidi.

Nadharia hii inagawanya matamko katika makundi mawili: tamko wazi/dhahiri na tamko fiche. Tamko wazi hutokana na hali ya kutokuwa na matamshi yenye utata/yenye maana nyingi. Nalo tamko fiche hutokana na uzulishaji: yaani, kulingana na Grice (1975:24), ni kule kumaanisha kitu fulani kwa kusema kitu kingine Kwa mfano:

(4) A: Unataka kucheza?

B: Nina maumivu.

Katika mfano (4) tamko wazi ni kuwa kwa wakati huo “B” ana maumivu kwa hivyo hawezi kucheza. Tamko fiche ni kuwa “B” hataki kucheza.

Ujumbe ukiwa wazi au fiche lazima ufasiriwe nayo nadharia hii inapendekeza mikakati ifuatayo mitatu ya kufasiri ujumbe:

Mkakati wa ubanaji ambapo dhana ambayo ni ya ukweli katika kundi la maneno huhusishwa katika kijikundi finyu cha kundi hilo. Hivyo basi utumiaji wa dhana huchukua tu vipengele ambavyo vinauhusiano nayo. Ubanaji hushirikisha kule kutumia neno kuwasilisha dhana dhahiri kuliko ile dhana iliyosimbwa. Kwa mfano:

- (5) i. John alisema anataka *kinywaji*.
- ii. Churchill ni *mwanamume*.

Katika mfano (5) neno husika linatumwiwa kuwasilisha maana dhahiri zaidi kuliko maana ya neno lenyewe. Katika (5i) maana inayojitokeza ni kuwa John angetaka pombe wala sio kinywaji

chochote kingine. (5ii) Neno mwanamume linawasilisha maana ya kuwa jasiri, kuwa tajiri, kuwa na wanawake wengi wala sio kuwa ni mtu wa jinsia ya kiume.

Katika mkakati wa upanuaji, kuna uwasilishaji wa dhana ambayo maana yake, katika muktadha mahususi, huwa ya kijumla kuliko ile iliyosimbwa kiisimu. Yaani kinachowasilishwa ni sehemu ya kilichosimbwa. Katika mkakati huu maneno hutumiwa kuwasilisha maana ya kijumla zaidi kuliko ile iliyosimbwa. Kwa mfano:

(6) Sally ni *kinyonga*.

Kinyonga ni aina ya mnyama. Neno hili limetumiwa kiistiari kwa kuwa Sally ambaye ni binadamu kwa hakika hawezi kuwa kinyonga. Kinachomaanishwa hapa ni kuwa Sally anamiliki tabia fulani za kinyonga. Sally ana tabia ya kubadilisha hulka zake katika mazingira tofauti anapoingiana na watu tofauti.

Mkakati wa ukadiriaji hushikilia kuwa, maneno yenyе maana halisi hupanuliwa kidogo ili kushirikisha vipengele ambavyo kwa uhakika havihusiani na maana halisi ya neno hilo. Kwa mfano:

(7) Sera hizi *zitawafilisisha* wakulima.

Neno filisisha linaweza kuchukuliwa kuwasilisha maana yake halisi au kuwasilisha kuwa na uhusiano wa karibu kimaana na neno filisisha. Hivyo basi tunaweza kufasiri kuwa sera hizo zitawaweka wakulima katika hali iliyo karibu na kafilisika.

Nadharia hii inashikilia kuwa katika michakato ya kufasiri ujumbe wasemewa huchukulia kuwa msemaji ametamka sentensi yenyе maana fulani ya kiisimu kama dokezo la lengo la msemaji. Hivyo basi yeye hutumia utaratibu ufautao ili kufikia uamuzi kuhusu maana lengwa ya msemaji (utaratibu wa ufahamu katika nadharia ya uhusiano):

- a) fuata mkondo wa mchakato mdogo katika kujenga ufasiri wa tamko. Tathmini nadharia tete fasiriwa (maana fiche mbalimbali, utatuzi wa warejelewa) kwa namna ambavyo nadharia hizo tete zitapatikana.
- b) acha ikiwa matarajio yako (msemewa) ya uhusiano yametoshelezwa.

Kulingana na utaratibu huu msemaji ambaye ananuia tamko lake lieleweke kwa urahisi iwezekanavyo lazima aliweke kwa namna ambavyo ufasiri wa kwanza ambao utatosheleza matarajio ya uhusiano ya msemewa ndio ule aliolenga kuwasilisha.

Utaratibu wa kusimba viwakilishi uliopendekezwa na Sperber na Wilson (1993) una manufaa kwa sababu hupunguza gharama ya michakato kwa msemewa wakati ambapo anatafuta uhusiano wa tamko ambalo analifasiri. Viwakilishi husimba taratibu zenyenye vikwazo kwenye kauli lililotamkwa. “Mimi” husimba maagizo ya kitaratibu kwa msemewa kutafuta mrejelewa kwanza kwa kutambua msemaji. Kwa hivyo viwakilishi husimba maagizo ya kitaratibu ambayo humsaidia msemewa kupata umbo la propozisheni la tamko. Kwa mfano:

(8) A: *Mimi ni mgonjwa. (Mwanafunzi kwa mwalimu)*

Katika mfano (8) “mimi” ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza katika umoja. Kiwakilishi hiki kinamrejelea msemaji wa tamko hili.

Utaratibu wa kusimba viwakilishi “Mimi/Ni” kulingana na nadharia hii ni: *kutambua kirejelewa kwanza kwa kumtambua msemaji*. Msemaji ni mwanafunzi.

Kulingana na utaratibu wa ufahamu katika nadharia ya uhusiano hatua zifuatazo za uzulishaji zilipitia akilini mwa msemewa:

- (a) “A” ametamka tamko lenye umbo la kimantiki.
- (b) Kutohana na udhaniaji wa uhusiano, tamko la “A” lina uhusiano unaofaa zaidi.
- (c) Viwakilishi katika tamko la “A” linapata uhusiano kwa namna fulani kwa kuwa limeashiria mtu anayejitokeza wazi katika muktadha huu.
- (d) Mimi ni mgonjwa (Maana kitaratibu ya viwakilishi- *tambua kirejelewa kwanza kwa kumtambua msemaji*).
- (e) Mtu anayeashiriwa na “mimi” ni msemaji ambaye ni mwanafunzi katika umbo la kipropozisheni.

Nadharia hii ilitufaa katika utafiti huu kwa sababu ufasiri wa maneno ya kiusonde hutegemea muktadha wa matumizi, nadharia hii nayo inahusu ufasiri wa maana katika muktadha mbalimbali. Katika uchunguzi huu tuliweza kutathmini matamko katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi kwa kurejelea utaratibu wa kusimba viwakilishi na utaratibu wa ufahamu katika nadharia ya uhusiano.

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii

Habwe na Karanja (2004) wamefafanua dhana ya usonde pamoja na kutueleza kategoria tano za usonde katika lugha ya Kiswahili ambazo ni: *usonde nafsi* kama vile ‘mimi’, ‘wewe’, ‘yeye’, ‘wao’, *usonde wakati* kama vile ‘sasa’, ‘kesho’, ‘leo’, ‘baadaye’, ‘mtondogoo’, ‘jana’, ‘juzi’, *usonde jamii* ambapo tungo hutegemea mahusiano ya kijamii kama vile ‘mama’, ‘shangazi’, ‘rais’, ‘mzee’ ‘mjomba’, *usonde diskosi* amba ni urejelezi ulio ndani mwa makala, na *usonde mahali* kama vile ‘humu’, ‘hapo’, ‘pale’, na ‘hapa’. Kazi hii ilitufaa kwa sababu utafiti huu ulishughulikia usonde katika lugha ya Kiswahili na kwa hivyo tuliweza kubainisha namna ambavyo usonde jamii na usonde nafsi hujitokeza katika lugha ya Kiswahili.

Marmaridou (2000) ameeleza njia fafanuzi za usonde, kategoria za usonde na matatizo yanayotokana na uhakiki wa usonde. Muhimu, kwetu sisi, katika kazi hii ya Marmaridou ni mtazamo wake kwamba usonde nafsi na usonde jamii haziwezi kujadiliwa kikamilifu bila kurejeleana. Marmaridou anaeleza kuwa wakati wowote amba kategoria hizi mbili za usonde zitakutana au kupishana usonde jamii hutumika kama sifa muhimu ya ziada ya usonde nafsi (Marmaridou, 2000:81). Mtazamo huu ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu lengo letu moja ni kuchunguza iwapo kuna uwiano baina ya usonde hizi mbili.

Filmore (1971) ameshughulikia usonde wakati na usonde mahali pamoja na kuzihusisha usonde nafsi na usonde jamii. Ameeleza kuwa mahali pa kutafutia habari kuhusu usonde jamii katika lugha yoyote ile ni pamoja na: mbinu za kuonyesha nafsi kama vile katika lugha ya Kiingereza na lugha nyingine; njia mbalimbali za kutenganisha viwango vya usemi kama vile tofauti kati ya usemi wenye heshima, wenye upole na usemi wazi; namna ya kutofautisha misemo mbalimbali kulingana na sifa fulani za wahusika katika vitendo usemi kama vile ikiwa ni usemi wa

mwanamume hadi mwanamume mzima, mwanamke hadi mwanamume, mtu ye yeyote mzima hadi mtoto au mtoto hadi mtu ye yeyote mzima (Filmore, 1971:75)

Kazi hii, kama ya Marmaridou, ilitufaa katika utafiti wetu kwa sababu tulichunguza iwapo kuna uwiano kati ya aina hizi mbili za usonde.

Levinson (1983) ameeleza usonde nafsi na usonde jamii kama kategoria mbili tofauti. Kulingana naye usonde nafsi huhusu kusimba washiriki katika vitendo usemi ambamo unenaji husika umetolewa na ambao huonekana moja kwa moja katika kategoria za kisarufi za nafsi ambazo ni nafsi ya kwanza, pili au ya tatu. Levinson ameeleza kuwa usonde jamii huhusu uonyeshaji wa mahusiano ya kijamii katika matamshi ya kiisimu pamoja na kuhusisha matamshi haya na hadhi za kijamii au majukumu ya washiriki katika tukio la mawasiliano. Hata hivyo, Levinson anasema kuwa wakati mwengine usonde jamii hujitokeza katika usonde nafsi inaposhirikishwa na tofauti za hadhi za kijamii kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

Mawazo haya ya Levinson yalitufaa pia katika kuchunguza nafasi ya usonde jamii katika usonde nafsi.

Otwere (2011) ameshughulikia usonde katika tafsiri. Katika kazi yake ameonyesha namna ambavyo manbe kutoka kwa lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahilieno ya usonde huweza kuathiri tafsiri ya ujumbe kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Kazi hii ilitufaa kwa sababu tuliweza kubainisha maneno ya usonde yanavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili.

1.9 Njia za Utafiti

Data iliyokusanywa ilikuwa matamshi ya usonde nafsi na usonde jamii katika mazungumzo ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika Shule ya Upili ya Xaverian na kuhusisha ufasiri wa matamshi hayo na nadharia ya uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1986/1995 na 1993).

Tuliamua kufanya utafiti wetu katika shule moja kwa sababu ya wakati. Kwa kuwa tulifanya uchunguzi wa kina kuhusu usonde nafsi na usonde jamii na ufasiri wao utafiti wetu utakuwa wa kifani.

1.9.1 Aina ya Utafiti

Njia iliyotumiwa katika utafiti huu ilikuwa ya utafiti kimaelezo kwa sababu aina hii ya utafiti hueleza hali ya matukio ilivyo kwa wakati uliopo. Kothari (2004) anaeleza kuwa njia hii ya utafiti hutumika pia katika utafiti kifani na utafiti wiano. Uchunguzi wetu ni wa kifani kwa kuwa tutachunguza mazungumzo baina ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika Shule ya Upili ya Xaverian, Kisumu.

Utafiti stahilifu pia ultumika kwa sababu data iliyochambuliwa ilikuwa ya kimatamshi. Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza kuwa data katika utafiti stahilifu huwa katika umbo la maneno wala sio la kinambari.

1.9.2 Data na Njia za Kukusanya Data

Kiini cha data iliyotumiwa ni mazungumzo kati ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili. Katika mazungumzo hayo, ambayo yalikuwa kwa lugha ya Kiswahili, tulijikita kwa matamshi yenye usonde na ufasiri wao.

Data iliyokusanya ilikuwa ya kimsingi kwa sababu ilikusanya moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa; walimu na wanafunzi, katika uwanja wa utafiti; Shule ya Upili ya Xaverian (Kothari, 2004:95).

Data ilikusanya kwa njia ya kushiriki, kusikiliza na kuandika. Njia hii ilitufaa kwa sababu kulingana na Kothari (2004) data inayokusanya kwa njia hii huhuishwa moja kwa moja na matukio katika wakati uliopo; yaani data hii haiathiriwi na tabia za awali au makusudio ya baadaye ya washiriki.

Kinasa-sauti kilitumiwa pia katika kukusanya data kama njia mahususi ya kuhifadhi data hizo. Njia hii ilitufaa kwa sababu ilituwezesha kuchunguza mazungumzo baina ya walimu na wanafunzi wao kwa kina hata baada ya mazungumzo hayo.

Kwa hivyo hatua zilizotumiwa katika kukusanya data ziliwa kushiriki, kusikiliza na kuandika, na kurekodi. Mtafiti baadaye alichagua matamshi ambayo yana usonde nafsi na usonde jamii.

1.9.3 Idadi ya Watafitiwa na Sampuli

Mugenda na Mugenda (2003) wamefafanua idadi ya watafitiwa kuwa ni ile idadi jumla ya vikundi, vitu au matukio ambayo yana sifa bainifu zinazofanana. Katika utafiti wetu idadi jumla ya watafitiwa ni walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika Shule ya Upili ya Xaverian.

Sampuli kulingana na Mugenda na Mugenda (2003) ni sehemu ndogo ya idadi jumla ya utafiti. Sampuli maksuudi (isioelekezi), ambayo ni sampuli iliyochaguliwa kimaksudi na mtafiti kulingana na malengo ya utafiti wake, ilihuushwa katika utafiti huu. Sampuli yetu ilikuwa wanafunzi wa kidato cha nne na cha tatu. Vidato hivi vina madarasa manne: kidato cha nne kina madarasa mawili na cha tatu vilevile kina madarasa mawili. Kila darasa lina wanafunzi arobaini na watano.

Walimu wa Kiswahili katika shule hii ni watatu. Walimu hawa, ambao ni wanawake wawili na mwanamume mmoja, ndio walimu wa madarasa haya kwa hivyo wote watatu walishirikishwa katika utafiti huu.

1.9.4 Njia za Kuchambua Data

Data zilichambuliwa kwanza kwa kuthibitisha ikiwa matamshi ni ya usonde nafsi na usonde jamii pamoja na kuthibitisha kama matamshi hayo yanaingiliana kwa kuzingatia mtazamo wa Marmaridou (2000).

Utaratibu wa kusimba viwakilishi na hatua za uzulishaji katika nadharia ya uhusiano zitatumiwa kuchanganua maneno ya usonde ili kubainisha ufasiri wao.

1.10 Muhtasari wa Sura

Tasnifu hii ina sura zifuatazo:

Sura ya Kwanza: Sura hii ina utangulizi, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada hii na njia za utafiti.

Sura ya Pili: **VIPENGELE MUHIMU KATIKA USONDE**
 Sura hii inashughulikia vipengele muhimu katika dhana ya usonde. Vipengele hivi ni kiini cha usonde, anafora, muktadha, matumizi ya usonde na matamko.

Sura ya Tatu: **USONDE NAFSI NA USONDE JAMII KATIKA KISWAHILI**
 Sura hii inashughulikia usonde jamii na usonde nafsi na namna ambavyo kategoria hizi za usonde zinajitokeza katika lugha ya Kiswahili.

Sura ya Nne: **UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA**
 Sura hii inashughulikia uchanganuzi wa data iliyokusanywa kwa kubainisha matamshi yenyenye usonde nafsi na usonde jamii na kuya tathmini kwa msingi wa uhusiano.

Sura ya Tano: **HITIMISHO NA PENDEKEZO**
 Sura hii inajikita katika kutathmini matokeo, malengo na nadharia tete ya utafiti. Hitimisho na mapendekezo.

SURA YA PILI

VIPENGELE MUHIMU KATIKA USONDE

2.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua dhana ya usonde na vipengele mbalimbali katika dhana ya usonde. Vipengele hivyo ni kiini cha usonde, anafora, suala la muktadha na umuhimu wake, matumizi ya usonde na tofauti kati ya sentensi na tamko. Mbali na sura hii kutufafanulia vipengele hivi muhimu vyatia usonde tunaweza kubainisha wakati ambapo maneno ya usonde yanafanya kazi ya usonde na wakati hayafanyi kazi hiyo.

Kwa sababu ufasiri wa maneno ya usonde hutokea katika muktadha wa matamshi tunafafanua dhana ya muktadha katika matamko. Utafiti wetu unahu matamshi ya usonde kwa hivyo tunatofautisha kati ya sentensi na tamko. Sura hii pia inatuonyesha wakati ambapo maneno ya usonde huhitaji na kutohitaji kuambatana na ishara.

Kwa kawaida katika mawasiliano msemaji hubadilika na kuwa msemewa naye msemewa akawa msemaji. Jambo hili hujitokeza mara kwa mara katika dhana ya usonde. Hivyo basi sura hii inatufafanulia kuhusu ubadilishanaji huu kati ya msemaji na msemewa katika kiini cha usonde.

2.2 Dhana ya Usonde

Usonde hushughulika na uhusiano uliopo baina ya matini na hali ambayo matini hiyo imetumiwa. Rankema (1993: 76) anaeleza kuwa usonde hutumiwa kutambua vipengele vyatia lugha ambavyo hurejelea moja kwa moja hali ya matumizi ya vipengele hivyo. Hii inamaanisha kuwa kile ambacho wasemaji au waandishi wanataka wakati mwengine hakilingani na mtazamo wa wasikilizaji na wasomaji. Kwa hivyo ni muhimu kufafanua maneno ya usonde ili kusawazisha mtazamo wa msemaji na msemewa au msomaji na mwandishi. Usonde kwa hivyo huonyesha uhusiano ulipo baina ya tamko la kiisumu na muktadha wake kwa kutambua msemaji na msemewa (msikilizaji), mahali na wakati wa matamshi.

Kulingana na Marmaridou (2000) usonde ni hali ya kutumia matamshi fulani ya kiisimu ili kufahamu maana katika muktadha wa kiwakati, mahali, jamii na mazungumzo. Marmaridou anaeleza kuwa matamshi ya usonde yana vipengele vya vitendo usemi kwa hivyo hayawezi kufasiriwa kikamilifu bila ya kushirikisha vigezo vya kimuktadha.

Fillmore (1971) anaeleza kuwa maneno ya usonde yanaweza kufasiriwa ikiwa tu sentensi ambazo maneno hayo yanapatikana zinaeleweka kuwa zimeegemezwa kwenye muktadha fulani wa kijamii. Anaeleza kuwa muktadha huo lazima ufanuliwe kwa namna ambavyo washiriki katika vitendo mawasiliano watatambuliwa, pamoja na wakati na mahali ambapo kitendo mawasiliano kilitendeka.

Usonde humaanisha kuashiria kupitia lugha (Yule, 1996). Yule kama Fillmore anaeleza kuwa ufasiri wa maneno ya usonde hutegemea msemaji na msikilizaji ambao wako kwenye muktadha unaofanana. Maneno ya usonde huwa na matumizi mengi ya kimsingi katika mazungumzo ya ana kwa ana. Kwa mfano “mimi” hueleweka kwa urahisi na wale walioko wakati wa matamshi kuliko wasiokuweko. Hii ni kwa sababu wataweza kumwona yule anayerejelewa kama “mimi”. Kulingana na Yule, kwa hivyo, maneno ya usonde huwa katika makundi mawili: yale yanayoonyesha hali ya kuwa “karibu na msemaji” na ‘mbali na msemaji’. (Ufanuzi wa hali hizi mbili umetolewa katika sehemu ifuatavyo [2.2]).

Kwa ujumla ufasiri wa maneno ya usonde hutegemea muktadha husika k.v. msemaji na msemewa, mahali na wakati wa matamshi. Hivyo basi usonde ni tamko linalopata maana yake katika muktadha ambao tamko hilo lilitamkwa.

2.3 Kiini cha Usonde

Kiini cha usonde huashiriwa na msemaji. Bühler (1934) anaeleza kuwa maneno ya usonde huweza kufasiriwa tu kupitia kiini cha usonde, dhana ambayo ameirejelea kama “origo”. Anachukulia kuwa kiini cha usonde ambacho ni msemaji hufafanuliwa na msemaji katika wakati na mahali pake pa matamshi. Kwa mfano vionyeshi “hapa” na “pale” katika lugha ya Kiswahili huweza kuonyesha sehemu mbili tofauti vikihusishwa na kiini cha usonde: “hapa” huonyesha

sehemu iliyio karibu na msemaji (ni sehemu iliyio kwenye kiini cha usonde) na “pale” huonyesha sehemu iliyio mbali na msemaji (sehemu hii haiko kwenye kiini cha usonde).

(9) “Ukisimama *hapa* utaweza kuona kijiji chetu.”

Katika (9) neno “*hapa*” linarejelea mahali mahususi ambapo msemaji yupo, kwa hivyo msemewa lazima afahamu mahali hapo ili aweze kufasiri kikamilifu kinachosemwa.

Katika lugha ya Kiswahili dhana ya umbali na ukaribu kwa kumzingatia msemaji huonyeshwa kwa kutumia vionyeshi kama ifuatavyo:

Jedwali 1: Vionyeshi

Msemaji	Vionyeshi				
	Viumbe wenyе uhai		Kitu au Hali		Mahali
	Umoja	Wingi	Umoja	Wingi	Umoja/Wingi
Karibu	Mtu huyu Mnyama huyu	Watuhawa Wanyama hawa	Kitihiki Ugonjwa huu	Viti hivi Magonjwa haya	Mahali hapa/humu/huku
Mbali kidogo (Katikati/karibu na msikilizaji)	Mtu huyo Mnyama huyo	Watuhao Wanyama hao	Kiti hicho Ugonjwa huo	Viti hivyo Magonjwa hayo	Mahali hapo/humo/kuko
Mbali sana	Mtu yule Mnyama yule	Watuwale Wanyama wale	Kitikile Ugonjwa ule	Viti vile Magonjwa yale	Mahali pale/mle/kule

Kiini cha usonde hushirikisha kwa kiwango kikubwa kiunzi (fremu) husiano cha urejeleo ambacho Levinson (1996) amekitofautisha na aina nyingine mbili za viunzi nya urejeleo (kiunzi asili na kiunzi kamili) kama ifuatavyo:

Kiunzi husiano cha urejeleo humweka msemaji kama kiini cha ufasiri. Kiunzi hiki cha uhusiano huonyeshwa na maneno ya usonde k.v. “mimi” na “wewe” na “hapa” na “pale”. Kwa mfano:

- (10) (a) Daudi yuko *kule*.
 (b) *Wewe unaweza kuniimbia?*

Levinson anaeleza kuwa kiunzi asili cha urejeleo pamoja na kiunzi kamili cha urejeleo havina uhusiano na dhana ya usonde. Kiunzi asili cha urejeleo huchukua kiini chake cha urejeleo kutoka kwa sehemu ambapo kitu fulani kipo.

- (11) (a) Mpira upo *mbele ya gari*.
 (b) *Kikombe kilianguka kushoto mwa mjomba.*

Kiini cha urejeleo katika kiunzi kamili cha urejeleo ni maumbo ya kijiografia k.v. milima, mito, mashariki, kusini n.k.

- (12) (a) Walikuwa wakienda *mashariki*.
 (b) *Nyumba yake iko kwenye mlima.*

Kiini cha usonde kinaipatia dhana ya usonde sifa ya ubinafsi. Hii ni kwa sababu msemaji, katika tamko lake, hujipa jukumu la kuhusisha kila kitu katika usemi huo na yeze binafsi (vitu hivyo humzunguka yeze). Kwa hivyo tamko huwa na ubinafsi kwa sababu jukumu la msemaji hubadilika kutoka msemaji mmoja hadi mwengine katika mazungumzo. Kwa mfano, “mimi” ya msemaji yeoyote humrejelea yeze mwenyewe wakati wa tamko lake.

Kutokana na maelezo hayo ni sawa kusema kuwa katika mazungumzo kiini cha usonde hubadilikabadilika baina ya wahusika wa mazungumzo hayo. Hii inamaanisha kuwa maneno k.v. “hapa” na “pale” na “mimi” na “wewe” huchukua maana tofauti yaktumiwa na wasemaji tofauti.

Kwa muhtasari kiini cha usonde hushikilia kuwa:

Mhusika mkuu katika vitendo usemi ni msemaji.

Mahali pa kuu ni alipo msemaji wakati wa tamko.

Wakati mkuu ni wakati ambao msemaji alitamka usemi fulani.

2.4 Matumizi ya Usonde

Maneno ya usonde huweza kutumiwa kwa njia mbili: njia ya kuonyesha na njia ya kiishara. Njia ya kuonyesha kulingana na Fillmore (1971) hurejelea matumizi ya maneno ya usonde ambayo kwayo maana huweza kufasiriwa kwa usahihi iwapo tu mtu anatazama sehemu fulani za mwili wakati wa mawasiliano.

(13) Simtaki *huyu* ninamtaka *huyu*.

Pasi na msemaji wa tamko (13) kuonyesha kwa kidole au kwa macho watu au kile anachorejelea kama “*huyu*” katika tamko lake, hatakuwa amefaulu katika lengo lake la mawasiliano.

Marmaridou (2000) anaeleza kuwa njia ya kiishara ni matumizi ya maneno ya usonde ambayo ufasiri wao huhitaji ufahamu wa kigezo cha wakati, mahali na cha kijamii katika vitendo usemi.

(14) *Mimi* ni mwalimu.

Kwa kumtambua msemaji katika tamko (14) ni rahisi kufasiri maana ya tamko hilo. Hapa hapana haja ya kutumia vidole (kwa mfano) kuonyesha mrejelewa.

Fillmore (1971) anaonyesha tofauti kati ya matumizi haya mawili ya maneno ya usonde kwa kutoa mifano ifuatavyo:

(15) Kidole *hiki*

(16) Chuo *hiki*

Kule kutaja tu “kidole hiki” hakutatosha kupertisha ujumbe kwa sababu msemewa atahitaji kuona ni kidole kipi hasa kinachozungumziwa kwa hivyo itambidi msemaji kuonyesha kidole rejelewa. Lakini tamko (16) halihitaji kuonyesha kwa njia yoyote ile. Hii ni kwa msingi wa kuwa tayari yuko kwenye chuo hicho wakati wa kutoa matamshi hayo. Hivyo basi tamko (15) linaonyesha matumizi ya maneno ya usonde yanayohitaji kuonyesha huku (16) likionyesha matumizi ya maneno ya usonde ambayo ni ya kiishara.

2.5 Anafora

Maneno hutumiwa kurejelea neno au kitu ambacho tayari kilikuwa kimetajwa awali katika matini au mazungumzo, hali ambayo huitwa anafora.

- (17) Maria hajafika ingawa *alitarajiwa* asubuhi.

Katika tamko (17) kiambishi “a” katika neno “alitarajiwa” ni kiambishi cha nafsi katika lugha ya Kiswahili pamoja na kuwa ni kiambishi kinachoonyesha usonde. Kiambishi hicho kinabainisha matumizi ya anafora kwa sababu kinamrejelea Maria.

Tofauti na maneno ya usonde, maneno ya anafora yanaweza kufasiriwa pasi na kuzingatia wakati na mahali katika muktadha wa mazungumzo. Ufasiri wa maneno ya anafora hutegemea maneno ambayo tayari yametajwa kwenye diskosi husika. Kwa mfano:

- (18) Niliendesha gari langu hadi Kisumu *nikaliacha huko*.

Kiambishi “li” katika neno “nikaliacha” ni anafora ya neno “gari” huku neno “huko” ni anafora ya neno “Kisumu”.

Kutokana na sifa ya anafora kuwa ni urejeleo wa neno ambalo tayari limetajwa katika matini au mazungumzo tunaweza kusema kuwa anafora ni njia ya kujiepusha na kule kurudiarudia maneno k.v.

- (19) Niliendesha gari langu hadi Kisumu *nikaacha gari langu Kisumu*.

Maneno ya usonde yanapotumiwa kuonyesha anafora katika tamko basi tena hayafanyi kazi ya usonde (Marmaridou, 2000). Kwa kurejelea mfano (18) “huko” ni kionyeshi cha mahali na huwa neno la usonde lakini katika mfano huo, neno hilo tena silo la usonde ila ni anafora.

2.6 Muktadha

Mawasiliano ni suala la kijamii kwa kuwa hutokea katika muktadha wa kijamii. Muktadha ni kipengele cha kijamii kwa sababu hujumlisha mfumo wa ndani wa jamii k.v. wahusika, uhusiano wao, mahala pa mawasiliano, njia ya mawasiliano pamoja na madhumuni ya mawasiliano.

Muktadha kwa ujumla ni mazingira ambamo jambo fulani hutokea (*Kamusi ya Karne ya 21, 2011*). Jambo ambalo ni muhimu katika utafiti wetu ni muktadha wa matamshi ambayo hujumuisha msemaji, msemewa, wakati na mahala pa matamshi.

(20) *Mimi* nina watoto.

Ili kuelewa tamko (20) lazima tumtambue anayezungumza kwa sababu neno “mimi” ni la usonde. Kwa kumtambua mimi ambaye anarejelewa tutakuwa tumefahamu mazingira ya tamko hilo na hivyo kufasiri maana yake kwa usahihi.

Kulingana na Leech (1983) muktadha ni ufahamu wowote walio nao msemaji na msikilizaji wake na ambao humsaidia msikilizaji kufasiri maana katika tamko la msemaji. Kwake Leech lazima msemaji na msikilizaji wake wawe na ufahamu unaofanana ili kuelewa na kufasiri tamko kwa usahihi.

Firth (1950) anatoa muhtasari kuhusu maelezo yake ya muktadha kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- a) Washiriki: anaeleza kuwa hawa ni watu na nafsi zao. Lyons (1977) amerejelea kigezo hiki kuwa ni majukumu na tabaka la washiriki. Washiriki huwa msemaji na msikilizaji wake katika tukio la mawasiliano.
- b) Matendo ya washiriki: Wanafanya nini wakati wa mawasiliano. Matendo haya yanashirikisha matendo ya kimaongezi na yale ya kiishara (yasiyo ya kimaongezi).

- c) Mambo mengine muhimu katika vitendo usemi: k.v. wakati, mahali n.k. na ikiwa yanaweza kuathiri kwa vyovvye vili hali ya tamko.
- d) Athari za vitendo usemi: ni mabadiliko yepi yalitokea baada ya tamko hilo.

Kinachojibainisha wazi katika sehemu hii ni kuwa ili kuweza kufasiri kwa usahihi maneno ya usonde lazima maneno hayo yashirikishwe na muktadha wa tamko. Hivyo basi lazima msemaji na msemewa wawe na ufahamu sawa wa muktadha huo ili kufanikisha mawasiliano. Muktadha ukibadilika basi maana ya maneno ya usonde hubadilika.

2.7 Matamko

Katika kuchunguza usonde tunajikita katika matamko ambayo hupata maana kutokana na muktadha wake wa utendi. Ni muhimu hivyo basi kuonyesha tofauti iliyopo kati ya tamko na sentensi.

Ingawa hakuna tofauti bayana kati ya sentensi na tamko wanaisimu wametoa fafanuzi mbalimbali ambazo tumetumia kutofautisha vipengele hivi viwili.

Bloomfield (1946) amefafanua sentensi kuwa umbo kubwa kabisa katika uchanganuzi wa kisarufi. Ni umbo ambalo viambajengo vyake huwa vimeunganishwa kwa kutumia kanuni mbalimbali za kisarufi. Hivyo basi sentensi ni umbo ambalo limekamilika kisarufi.

Crystal (1991) kwa mujibu wa Obuchi na Mukhwana (2010) anaeleza kwamba kimapokeo sentensi ilielezwa kama kipashio cha kujieleza na ambacho kinasheheni fikra kamili. Sentensi ni umbo la kiisimu lililohuru na kikubwa zaidi kati ya maumbo mengine ya kiisimu ambayo hutumiwa kisarufi. Kwao Obuchi na Mukhwana sentensi ni tungo kubwa zaidi kumuundo na ambalo husheheni maana kamili.

Kwa upande mwingine tamko ni kila kitu ambacho kimesemwa na msemaji mmoja kabla ya mwingine kuanza kuzungumza. Matamko yana sifa za kimaongezi pamoja na sifa zisizo za kimaongezi (Lyons, 1977); hata kusema “mmh”, “aah” kunachukuliwa kuwa ni matamko.

Mweri (2010) anaeleza kuwa katika mazungumzo tamko ni kila nafasi ya kuzungumza aliyonayo mzungumzaji hasa tukielewa kuwa mazungumzo hutokea kwa zamu. Anatoa mfano ufuatao:

(21) A: Unaenda dukani?

B: Ndio.

Anaeleza kuwa (A) na (B) katika (21) ni matamko pamoja na kuwa ni sentensi. Maeleo haya anayatoa kwa msingi wa kuwa tamko laweza kuwa neno moja au zaidi ya neno moja. Maeleo haya yanashahibiana na wazo la Lyons (1977) ya kwamba sentensi hujumlishwa katika tamko.

Kulingana na maumbo pamoja na matumizi yao, sentensi hugawanywa katika makundi mbalimbali. Habwe na Karanja (2004) wamezitaja sentensi taarifa, sentensi agizi na sentensi ulizi kuwa baadhi ya makundi ya sentensi kulingana na wanasarufi mapokeo. Vivyo hivyo kunazo sentensi sahili, ambatano, changamano pamoja na sentensi ambatano-changamano. Kwa msingi huu wa makundi kuna aina mbalimbali za matamko k.v. tamko elezi, tamko amri n.k.

Tofauti kuu iliyoko kati ya sentensi na tamko ni kuwa sentensi ni maumbo ya kisarufi yanayoundwa kwa kuzingatia kanuni za sintaksia na semantiki ilhali tamko ni tendo usemi na hubainishwa katika uwanja wa pragmatiki.

Wananadharia wa uhusiano Sperber na Wilson (1986/1995) wanashikilia kuwa lugha hufanya kazi mbili za kimsingi: kueleza na kufasiri. Katika kueleza lugha hutumia ukweli kama masharti huku katika kufasiri lugha hutumia ufananisho. Hivyo basi tamko ni ufasiri wa mawazo ambayo msemaji anataka kuwasilisha kwa hadhira yake.

Wananadharia hawa wanaeleza kuwa maana ya tamko ama huwa wazi (dhahiri) au fiche. Tamko wazi hutokana na hali ya kutokuwa na matamshi yenye utata/yenye maana nyingi. Nalo tamko lenye maana fiche hutokana na uzulishaji. Tamko hili ndilo ambalo Grice (1975) analirejelea kama kule kumaanisha kitu fulani kwa kusema kitu kingine. Kwa mfano:

(22) X: Unaweza kuendesha *mercedes*?

Y: Siwezi kuendesha gari lolote lenye bei ghali.

- a) “Y” hawezikuendesha gari lolote lenye bei ghali.

b) *Mercedes* ni gari lenye bei ghali.

c) “Y” hawezi kuendesha *mercedes*.

(22a) ni ufasiri uliowazi kwamba “Y” hawezi kuendesha gari lenye bei ghali. Ili kufikia uamuzi (22c) kuwa “Y” hawezi kuendesha Mercedes. “X” atapitia uzulishaji (22b) kuwa *Mercedes* ni gari lenye bei ghali kwa hivyo “Y” hawezi kuendesha *Mercedes* kwa sababu ni gari lenye bei ghali.

Kwa kuwa maana ya maneno ya usonde siyo ya moja kwa moja tunaweza kuyabainisha maneno hayo kuwa ni matamko yenyne maana fiche. Hii ni kwa sababu ufasiri wa maana humhitaji msikilizaji kufanya uzulishaji wa maneno hayo ili kupata maana sahihi. Kwa mfano:

(23) Wewe njoo hapa?

Maneno “wewe” na “hana” ni ya usonde. Ili kufasiri tamko hili kwa usahihi lazima tumjue msemaji na anayerejelewa kama “wewe” tena ni lazima tuwe na ufahamu wa mahali alipo msemaji ili kufasiri mahali panaporejelewa kama “hana”.

2.8 HITIMISHO

Sura hii imeonyesha mitazamo mbalimbali ya wataalamu kuhusu dhana ya usonde kuwa ni kule kutumia lugha kuashiria. Hivi kwamba ufasiri hutegemea muktadha.

Katika sura hii tumeeleza kiini cha usonde na umuhimu wake katika ufasiri wa maana ya maneneo ya usonde. Kimsingi kiini cha usonde huashiriwa na msemaji kwa kuzingatia msemaji mwenyewe, wakati na mahala pake pa matamshi (mimi, sasa na hapa). Tumeangazia namna ambavyo kiini cha usonde huchangia katika suala la ubinafsi katika usonde.

Namna ambavyo maneno ya usonde hutumika pia imeangaziwa katika sura hii. Tumeonyesha migao miwili ya matumizi haya: kuonyesha na kuashiria (ishara). Tumegundua kuwa matamshi mengine ya usonde humhitaji msemaji kutumia viungo mbalimbali vyta mwili ili tamko lake liweze kufasiriwa kwa usahihi. Wakati huo huo matamshi mengine humhitaji tu msikilizaji kujua wakati na mahala pa matamshi ili kufanya ufasiri wake.

Jambo lingine muhimu ambalo limeshughulikiwa ni anaphora ambalo limetuwezesha kutambua wakati maneno ya usonde yanafanya kazi ya usonde na wakati ambao maneno hayo hayafanyi kazi hiyo.

Suala la muktadha ni muhimu katika usonde na sura hii imeonyesha vipengele muhimu vyatuzingatia katika kufafanua muktadha na jinsi ambavyo muktadha huathiri maana ya maneno ya usonde.

Hatimaye tumetofautisha sentensi na tamko pamoja na kueleza makundi mawili ya maana za tamko: fiche na wazi.

Sura hii imetuwekea msingi wa kuweza kujadili kwa kina kategoria mbili za usonde: usonde nafsi na usonde jamii, na namna ambavyo zinajitokeza katika lugha ya Kiswahili.

SURA YA TATU

USONDE NAFSI NA USONDE JAMII KATIKA KISWAHILI

3.1 UTANGULIZI

Sura hii inafafanua matumizi ya usonde nafsi na usonde jamii. Katika ufanuzi wetu tumetumia mifano kutoka kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa lugha hii ndiyo lugha tunayoitafitia. Tumeonyesha namna ambavyo maneno ya usonde nafsi na usonde jamii hujitokeza katika lugha ya Kiswahili.

3.2 USONDE NAFSI

Usonde nafsi hurejelea wahusika katika tukio la mawasiliano. Wahusika huwa msemaji ambaye huwa kiini cha usonde na msikilizaji (msemewa). Marmaridou (2000) anaeleza kuwa wahusika hubadilishana nafasi ya kuzungumza katika tukio la mawasiliano ambapo msemaji huwa msikilizaji na msikilizaji akawa msemaji. Kwa hivyo kutokana na hali hii usonde nafsi huchunguza majukumu ya wahusika katika tukio la mawasiliano.

3.2.1 Viwakilishi vya Nafsi

Viwakilishi vya nafsi hutumika kuonyesha maneno ya usonde katika matamko. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa viwakilishi hutumiwa badala ya nomino katika nafsi ya kwanza, pili na tatu. Katika Kiswahili viwakilishi hivi vya nafsi huwa huru na tegemezi (viambata) katika umoja na wingi. Jedwali lifuatalo linatoa muhtasari wa viwakilishi vya nafsi katika lugha ya Kiswahili.


Jedwali 2: Viwakilishi nya Nafsi

		Kiwakilishi		
Nafsi	Huru	Tegemezi		
	Umoja	Wingi	Umoja	Wingi
I	Mimi	Sisi	Ni-	Tu-
II	Wewe	Nyinyi	U-	M-
III	Yeye	Wao	A-	Wa-

Dhana ya kuwa mbali au karibu na msemaji katika tukio la mawasiliano, ambayo tulishughulikia katika sura ya pili inajitokeza hapa. Nafsi ya pili huwa karibu na msemaji huku nafsi ya tatu ikiwa mbali na msemaji au huonyesha mtu asiyekuwa wakati wa tamko fulani.

Kulingana na Lyons (1968) nafsi ya kwanza hutumiwa na msemaji kujirejelea yeye mwenyewe, nafsi ya pili humrejelea msikilizaji (msemewa) na nafsi ya tatu humrejelea mtu ambaye si msikilizaji wala msemaji katika tukio la mawasiliano. Mawazo haya ya Lyons yanaweza kuwasilishwa ifuatavyo katika mchoro huu:

Mchoro 1: Uhusika Katika Tukio la Mawasiliano



¹ +mhusika: wahusika katika tukio la mawasiliano.

² -mhusika: siye mhusika katika tukio la mawasiliano.

Kwa hivyo kulingana na Lyons nafsi ya tatu haihusiki moja kwa moja katika tukio la mawasiliano. Kwa mfano:

- (24) *Yeye ni mwalimu wetu.*

“Yeye” ni kiwakilishi nafsi ya tatu. “Yeye” hapa sio msemewa wala msemaji ni mrejelewa tu. Katika mfano (25) unaofuata tunaonyesha nafsi ya kwanza na pili zikiwa msemaji na msemewa mtawalia katika tukio la mawasiliano.

- (25) *Mimi na wewe ni marafiki.*

Mimi ni nafsi ya kwanza (msemaji) na wewe ni nafsi ya pili (msemewa).

Kiini cha usonde hubadilikabadilika baina ya wahusika katika tukio la mawasiliano. Kama tulivyoeleza awali “mimi” huwa msemaji na “wewe” huwa msemewa ambaye akipokea zamu ya kuzungumza atabadilika na kuwa “mimi” naye msemaji akabadilika na kuwa msemewa “wewe”. Tena katika ufasiri “mimi” huwa “wewe” na “wewe” huwa “mimi” kwa msemewa. Kwa mfano:

- (26) A: *Mimi nilicheza vizuri.*

B: *Mimi pia nilicheza vizuri.*

“A” na “B” katika mfano (26) ni wahusika katika tukio hili la mawasiliano. “A” ni msemaji na “B” ni msemewa. Vivyo hivyo “B” anabadilika na kuwa msemaji huku “A” akiwa msemewa. “Mimi” katika “A” inamrejelea “A” naye “B” ataifasiri kama “wewe” huku “mimi” katika “B” ikimrejelea “B” wala sio “A”, “A” ataifasiri kama “wewe”.

Maelezo haya yanaonyesha kuwa viwakilishi vinapotumiwa katika mazungumzo kuonyesha usonde, urejeleo hutegemea namna wazungumzaji wanavyobadilisha awamu ya majukumu ya msemewa na msemaji katika tukio la mawasiliano.

3.2.1.1 Nafsi ya Kwanza

Nafsi ya kwanza katika umoja humrejelea msemaji kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

- (27) *Mimi nitapika chakula.*

- (28) *Nimekujengea nyumba kubwa.*

Nafsi ya kwanza wingi “sisi” na “tu-” haitoi maana ya moja kwa moja ya kumrejelea msemaji peke yake. Fillmore (1971) anasema kuwa nafsi ya kwanza wingi haimaanishi wasemaji wengi kwa wakati mmoja wa uneni bali hutumiwa kuonyesha hali mbili zifuatazo:


Hali ya kwanza ni kule kumshirikisha msemaji na msemewa. Kwa mfano:

- (29) *Tuelekee darasani pamoja.*

- (30) *Sisi, mimi na wewe, ndio wa kwanza kufika hapa.*

Msemaji katika matamko (29) na (30) anajirejelea yeye mwenyewe na msemewa (ambaye anamsemeza) hivi ni kwamba wamevitekeleza vitendo hivyo kwa pamoja. Matumizi haya ya nafsi ya kwanza wingi yameonyeshwa na Ingram (1971) kwa kutumia mchoro ufuatao:

Mchoro 2: Kushirikisha msemewa



“Sisi/tu [+msemewa]”

Hali ya pili ni pale ambapo nafsi ya kwanza wingi haimshirikisha msemewa lakini inamshirikisha mwingine ambaye si msemewa. Kwa mfano:


- (31) *Tulikuwa tukikusubiri uje nyumbani.*

- (32) *Sisi hatukutaki wewe hapa.*

³ - Mwingine: si msemaji wala msemewa; hashirikishwi katika nafsi ya kwanza wingi.

“Ku” ni nafsi ya pili inayoonyesha mtendewa katika mfano (31) na (32). “Ku” hapa ndiye msemewa kwa hivyo katika matamko haya hajashirikishwa katika “tu” na “sisi” katika (31) na (32) mtawalia. Yaani hayuko kwenye kundi la waliokuwa wakimsubiri wala wasiomtaka. Vipengele vya hali hii vinaonyeshwa kama ifuatavyo:

Mchoro 3: Kutoshirikisha msemewa



“sisi/tu [-msemewa]”

Levinson (1983) anaeleza kuwa wakati mwingine msemaji hashirikishwi katika nafsi ya kwanza wingi, hali ambayo hutokea kwa wingi katika miktadha ya daktari na mgonjwa na mwalimu na wanafunzi. Hali hii kwa hivyo huleta dhana ya msemaji kutaka kujiweka katika kiwango sawa na msemewa labda kwa kutaka kuziba tofauti za kitabaka kati ya msemaji na msemewa. Hivyo basi katika muktadha huu ni sawa kusema kuwa usonde nafsi una kipengele cha kijamii.


(33) *Leo tunajihisi vipi? (daktari kwa mgonjwa)*

(34) *Tukumbuke kubeba vitabu vya fasihi kesho. (mwalimu kwa wanafunzi)*

“Tu” (tamko 33) haimshirikishi daktari kwa sababu yeye si mgonjwa vivyo hivyo “tu” (tamko 34) haimshirikishi mwalimu. Uhusika wa hali hii ni kama ifuatavyo:

⁴ +Mwingine: si msemaji wala msemewa lakini ameshirikishwa katika nafsi ya kwanza wingi. Msemewa hajashirikishwa

Mchoro 4: Kutoshirikisha Msemaji



“Sisi/tu [-msemaji]”

3.2.1.2 Nafsi ya Pili

Nafsi ya pili humrejelea msemewa katika tukio la mawasiliano. Kwa mfano:

- (35) (a) *Wewe* ulienda nyumbani mapema sana. (umoja)
 (b) *Nyinyi* mlienda nyumbani mapema sana. (wingi)

Katika mfano (35a na 35b) “wewe” na “nyinyi” ni viwakilishi vyatya nafsi ya pili katika umoja na wingi mtawalia.

Nafsi ya pili wingi huweza kutumiwa kuonyesha msemewa na mtu mwengine ambaye si msemaji wala msemewa kama vile:


- (36) Wewe na Okwenga *mlichelewa* kufika kazini.

“M” ni kiwakilishi nafsi kiambata cha nafsi ya pili na katika muktadha huu kiwakilishi hiki kinamrejelea msemewa “wewe” na “Okwenga” ambaye si msemewa wala msemaji. Uhusika wa hali hii unaweza kuonyeshwa kama ifuatavyo:

⁵ -msemaji: msemaji hajashirikishwa.

⁶ \pm Mwingine: si msemaji wala msemewa, anaweza kushirikishwa au asishirikishwe.

Mchoro 5: “Mwingine” Katika Nafsi ya Pili Wingi



Kulingana na Marmaridou (2000) nafsi ya pili wakati mwingine inapotumika msemewa hawezi kutambuliwa kwa njia wazi: haijulikani moja kwa moja nani hasa ni msemewa katika tamko. Mara nyingi hali hii hujitokeza katika matangazo. Kwa mfano:

- (37) *Ukinunua mbili utapewa moja bure.*

“U” katika (37) haimrejelei msemewa (msikilizaji) mahususi lakini mtu yejote ambaye atasikia au kusoma tangazo hilo atakuwa msemewa. Mfano mwingine ni katika maagizo k.v. ya upishi.

- (38) *Ukoroge mchanganyiko kwa dakika tatu.*

Atakayechagua kusoma maagizo hayo au kuyasikiliza labda kwenye redio au runinga atakuwa msemewa. Katika matumizi haya ya nafsi ya pili sifa muhimu ya usonde nafsi ambayo ni mawasiliano ya ana kwa ana hypotea.

Hata hivyo katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi ambayo huwa na maagizo msemewa hutambuliwa wazi: ni mwanafunzi.

⁷ –msemaji: msemaji hajashirikishwa.

⁸ +Mwingine: si msemaji wala msemewa, ameshirikishwa katika nafsi ya pili wingi.

3.2.1.2.1 Kauli za Mnenei

Kauli za mnenei ni mifano mizuri sana ya usonde (Levinson, 1983). Kauli za mnenei ni mbinu za kiisimu ambazo hutumiwa na msemaji kumtambua msemewa katika tamko. Nafsi ya pili hutumiwa kuonyesha kauli za mnenei. Kwa mfano:

(39) *Wewe, umekwaruza gari langu.*

(40) *Nyinyi, mjaribu kumaliza kazi zenu.*

“Wewe” na “nyinyi” katika tamko (39) na (40) mtawalia ni kauli za mnenei ambazo zimetumiwa kuleta dhana ya kusistiza kuwa msemaji anazungumza na mtu fulani: “ni wewe ninayezungumza naye wala sio mwengine.” Viwakilishi nafsi hivi ni kauli za mnenei ambazo zimetumika kunasa makini ya msemewa.

Kunazo aina mbili za kauli za mnenei: visemewa na mwito. Visemewa hutokea katikati au mwishoni mwa tamko huku mwito ukiokea mwanzoni mwa tamko. Mwito huambatana na kuonyesha (ishara) ingawa visemewa havihitaji kuonyesha (taz. matumizi ya usonde uk 19). Kwa mfano:

(41) *Nendeni dukani, nyinyi. (kisemewa)*

(42) *Nyinyi, nendeni dukani. (mwito)*

Muhimu kuhusu kauli za mnenei ni kuwa kauli hizi huwa na vipengele vya kijamii. Huku ni kusema kuwa kauli hizi huonyesha mahusiano mbalimbali kati ya wahusika au hisia mbalimbali zinazojitokeza kwenye tukio la mawasiliano.

Nafsi ya pili ikitumiwa kwenye mwito huleta dhana ya ukali, amri na kuonyesha uhusiano baina ya wahusika (k.v. kuonyesha tofauti za kitabaka kati ya wahusika) kwenye tukio la mawasiliano. Kwa mfano:

(43) *Nyinyi, mbona hamjamaliza kazi zenu? (mwalimu kwa wanafunzi)*

(44) *Wewe, unatusumbua? (Mwanafunzi kwa mwalimu)*

Katika tamko (43) mwalimu anauliza wanafunzi wake swalii lakini kuna ukali katika tamko hilo. Labda amekasirishwa na wanafunzi hao kwa kutomaliza kazi fulani. Lakini tamko (44) haliwezi kuwa sawa kijamii kwa sababu jamii haitarajii ya kuwa mwanafunzi ataweba kumtamkia mwalimu tamko kama hilo. Ikiwa atafanya hivyo basi atakuwa amemkosea mwalimu heshima.

Mifano hiyo miwili pia inatuonyesha mahusiano baina ya wahusika hawa wawili (mahusiano ya mwalimu-mwanafunzi). Katika mahusiano hayo ni kuwa mwalimu anaweza kuonyesha ukali (anachukuliwa kuwa na hadhi ya juu) naye mwanafunzi ni sharti awe mnyenyeketu kwa mwalimu wake (ana hadhi ya chini).


Kutokana na maelezo yetu kuhusu nafsi ya pili na kauli za mneni tunaweza kusema kuwa usonde nafsi una uwiano na usonde jamii ambayo huonyesha mahusiano baina ya wahusika katika tukio la mawasiliano.

3.2.1.3 Nafsi ya Tatoo

Nafsi ya tatoo humrejelea mtu ambaye si msemaji wala msemewa katika tukio la mawasiliano, anaweza kuwa mrejelewa au hadhira isiyokuwa msemewa (Levinson, 1983).

Uhusika huu katika nafsi ya tatoo unaonyeshwa hivi:

Mchoro 6: Nafsi ya Tatoo



“Yeye/Wao”

Lugha nyingi za dunia kama vile Kiingereza hutumia nafsi ya tatoo kuonyesha jinsia. Kiswahili ni tofauti kabisa kwa sababu viwakilishi vyake vya nafsi ya tatoo havionyeshi jinsia. Viwakilishi hivyo huwa “yeye” (umoja) na “wao” (wingi) pamoja na viambata vyao “a-” (umoja) na “wa-” (wingi). Kwa mfano:

(45) Alitaka kucheza lakini *wao* walikataa.

“A” – Kiwakilishi kiambata cha nafsi ya tatu umoja katika Kiswahili.

“Wao” – Kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu wingi katika Kiswahili.

Kutokana na mfano wetu (45) tunabainisha kuwa lugha ya Kiswahili haina viwakilishi nya kuonyesha jinsia moja kwa moja kama ilivyo katika lugha ya Kiingereza. Labda kwa kutaka kuonyesha jinsia katika tamko hilo msemaji atalazimishwa kutaja majina mahususi ya jinsia katika uneni wake. Anaweza kusema hivi:

(46) Yeye, *Kristina*, alitaka kucheza lakini wao walikataa.

Kwa kumtaja Kristina, msemaji atakuwa ameonyesha jinsia ya kike. Suala la jinsia ni suala la kijamii kwa hivyo iwapo msemaji atakuwa na lengo la kuonyesha jinsia katika tamko lake basi atakuwa akiihusisha usonde nafsi na usonde jamii.

Marmaridou (2000) anashikilia kuwa nafsi ya tatu ni njia hafifu ya kuonyesha usonde kwa sababu nafsi hii haimwonyeshi msemaji wala msemewa katika tukio la mawasiliano. Hata hivyo anaeleza kuwa katika miktadha mingine ya kijamii nafsi ya tatu huweza kuwa msemewa. Anatoa mfano ufuatao:

(47) Lazima Jonny aende kulala saa hii.

Anaeleza kuwa tamko hili linatokea katika muktadha wa kifamilia ambapo mzazi kwa kutaja nomino ya pekee Jonny (ambayo kwenye tamko hili liko katika nafsi ya tatu) atakuwa ameiweka nomino hiyo katika kundi la msemewa. Hapa tena tunaona kigezo cha jamii kikijitokeza katika matumizi ya usonde nafsi.

Hata hivyo katika lugha ya Kiswahili viwakilishi nafsi ya tatu havihitaji kigezo cha jamii ili kuonyesha usonde. Kwa mfano:

(48) Atafika mapema.

(49) *Wat*afika mapema.

“A” na “wa” ambavyo ni nafsi viambata ni vya usonde kwa sababu katika muktadha huu kutakuwa na haja ya kumjua anayerejelewa kama “a” na “wa” kwenye kufasiri ujumbe wa tamko hili. Wakati mwingine msemaji huweza kutumia kidole ama njia nyingine kuonyesha yule ambaye anamrejelea hivyo basi atakuwa amemshirikisha mtu huyo katika muktadha wa tamko.

3.2.2 Viwakilishi Vimilikishi

Viwakilishi hivi huzua dhana ya “kuwa na”. Yaani huonyesha kuwa kitu fulani kinamilikiwa na mtu fulani. Mofimu {-angu}, {-etu}, {-ako}, {-enu}, {-ake} na {-ao} hutegemea nafsi na hutumiwa pamoja na upatanisho wa kisarufi wa ngeli kuunda viwakilishi vimilikishi (Habwe na Karanja, 2004). Jedwali lifuatalo linatuonyesha vimilikishi hivi pamoja na nafsi zinazohusishwa navyo.

Jedwali 3: Nafsi na Vimilikishi

	Umoja		Wingi	
	Nafsi	Kimilikishi	Nafsi	Kimilikishi
I	Mimi	-angu	Sisi	-etu
II	Wewe	-ako	Nyinyi	-ako
III	Yeye	-ake	Wao	-ao

Jedwali lifuatalo linaonyesha namna ambavyo ngeli hushirikishwa katika vimilikishi pamoja na nafsi.

Jedwali 4: Ngeli, Nafsi na Vimilikishi

Ngeli	Umoja			Wingi		
	Nafsi	Kimilikishi	Sentensi	Nafsi	Kimilikishi	Sentensi
U-I	Mimi	-angu	Wangu umefungwa	Sisi	-etu	Yetu imefungwa
LI-YA	Wewe	-ako	Lako linapendeza	Nyinyi	-ako	Yenu yanapendeza
KI-VI	Yeye	-ake	Chake kimepotea	Wao	-ao	Chao kimepotea

Viwakilishi hivi huwa maneno ya usonde kwa sababu kwa kusema (kwa mfano) “lako limeharibika” ni vigumu kubainisha kinachorejelewa na “lako” ikiwa muktadha wa usemi hautazingatiwa. “Lako” laweza kuwa shati, gari au hata basi. Mfano ufuatao unatufafanulia zaidi kuhusu namna vimilikishi huwa maneno ya usonde.

(50) *Yangu ni kubwa kuliko yake.*

Katika kulifasiri tamko (50) vipengele vyta kimuktadha lazima vizingatiwe: msemaji na msemewa ni nani, ni nini anachokirejelea kama “yangu” na anayemiliki “yake” ni nani? “Yangu” ni kimilikishi cha nafsi ya kwanza umoja ambayo hapa ni msemaji na “yake” ni kimilikishi cha nafsi ya tatu umoja. Msemaji anaweza kuonyesha kwa kutumia vidole au njia nyingine zozote kama vile kutumia macho kuonyesha anayemiliki “yake”.

Ikumbukwe ya kuwa “yangu” ya msemaji ni tofauti na “yake” ya mtu huyu wa tatu. Hata kama msemaji alikuwa akizungumzia labda maembe, maembe ya msemaji siyo maembe ya mtu huyo wa tatu. Hii ndio sababu ya kuviweka vimilikishi katika kundi la maneno yenye usonde.

(51) Mwalimu anakuita.

(52) Mwalimu *wako* anakuita.

Katika tamko (51) msemaji na msemewa labda wana mwalimu mmoja ambaye wote wawili wanamjua, lakini katika tamko (52) msemaji ametumia kimilikishi “wako” kuonyesha kuwa

mwalimu wa msemewa ni tofauti na mwalimu wake au kuwa yeye si mwanafunzi labda ni mzazi anayetamka maneno haya kwa mwanawe ambaye ni mwanafunzi.

Katika maelezo ya hapo juu suala la mahusiano linajitokeza. Tukumbuke kuwa awali tumetaja ya kwamba mahusiano huonyeshwa katika usonde jamii. Kwa hivyo vimilikishi huweza kutumiwa kuonyesha wiano uliopo baina ya usonde nafsi na usonde jamii. Kwa mfano:

(53) Mama amewasili.

(54) Mama yangu amewasili.

Msemewa akiwa anazungumza na mtu kutoka kwa familia yake k.v. baba, dada au hata ndugu yake atatamka tamko (53). Lakini ikiwa anazungumza na mtu ambaye hatoki katika familia yake labda anazungumza na rafiki yake atatamka tamko (54) kuonyesha kuwa yeye na msemewa wana mama tofauti: mama yake siye mama wa rafiki yake.

3.2.3 Viwakilishi Virejeshi

Kulingana na Habwe na Karanja (2004) viwakilishi virejeshi hurejelea nomino kwa kuelezea juu ya kitendo fulani kilichotendwa na nomino hiyo. Virejeshi hivi hutumia mofu {o} rejeshi katika kitenzi au “amba-” pamoja na viambishi vya mwisho kulingana na ngeli husika kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali 5: Ngeli na Viwakilishi Virejeshi

Ngeli	Ambo- Rejeshi		O- Rejeshi	
	Umoja	Wingi	Umoja	Wingi
A-WA	<i>Ambaye</i> anacheza	<i>Ambo</i> wanacheza	Anayacheza	Wanaocheza
U-I	<i>Ambo</i> umeanguka	<i>Ambo</i> imeanguka	Uliaoanguka	Iliyoanguka
LI-YA	<i>Ambo</i> linauma	<i>Ambo</i> yanauma	Linalouma	Yanayouma
KI-VI	<i>Ambo</i> kitaletwa	<i>Ambo</i> vitaletwa	Kitakacholetwa	Vitakavyoletwa
I-ZI	<i>Ambo</i> imeungua	<i>Ambo</i> zimeungua	Iliyoungua	Zilizoungua
U	<i>Ambo</i> unaudhi		Unaoudhi	
U-YA	<i>Ambo</i> unaua	<i>Ambo</i> yanaua	Unaoua	Yanayoua

Virejeshi hivi vinapotumiwa pamoja na nomino katika tamko vinakoma kuwa maneno ya uso nde na kuwa na matumizi ya anafora. Kwa mfano:

- (55) (a) Mwanafunzi *ambaye* anaandika alinunua kalamu mpya.
(b) Mwanafunzi *anayeandika* alinunua kalamu mpya.

“Ambaye” na “ye” katika (55a) na (55b) mtawalia ni virejeshi. Virejeshi hivi siyo maneno ya usonde bali ni ya anafora. Hii ni kwa sababu vinarejelea nomino “mwanafunzi” ambayo tayari imetajwa kwenye tukio la mawasiliano. Anafora ni hali ambayo inajitokeza kwenye matini au mazungumzo wakati ambapo neno linatumwiwa kurejelea kitu au mtu ambaye alikuwa ametajwa awali kwenye matini husika (taz. anafora uk 20).

Kule kutumia virejeshi hivi pasi na nomino huviingiza virejeshi hivyo katika kundi la maneno ya usonde. Kwa mfano:

- (56) (a) *Ambaye* anaandika alinunua kalamu mpya.
(b) Anayeandika alinunua kalamu mpya.

Ufasiri wa tamko (56a) na (56b) utahitaji msemewa kumtambua anayerejelewa na virejeshi hivyo: ‘ni nani huyu ambaye anaandika’ ndilo swali ambalo msemewa atajiuliza katika ufasiri wake.

3.3 USONDE JAMII

Fillmore (1971) anafafanunua usonde jamii kuwa ni kule kuchunguza vipengele vyatya sentensi ambavyo huonyesha vigezo mbalimbali vyakijamii katika tendo usemi. Mbinu za kumtambua mtu, njia mbalimbali za kutofautisha viwango vyatya usemi (kwa mfano: usemi wenye upole, heshima, unyenyekevu n.k.) na namna mbalimbali ambavyo majina mahususi ya ukoo na ya vyeo hutofautiana katika maumbo na matumizi kulingana na uhusiano baina ya msemaji, msemewa, hadhira na mrejelewa ni baadhi ya mambo yanayohusika na usonde jamii.

Levinson (1979) anachukulia usonde jamii kuwa ni vipengele katika muundo wa lugha ambavyo vimeegemeza kwenye vitambulisho vyakijamii ambavyo hutumiwa kutambua wahusika katika tukio la mawasiliano au mahusiano baina ya wahusika hao na warejelewa wengine. Usonde jamii huhusu kutambua mahusiano ya kijamii katika matamko kwa kurejelea hadhi au majukumu ya wahusika katika tukio la mawasiliano.

Ufafanuzi wa Habwe na Karanja (2004) unalingana na ule wa Levinson kuwa maana ya tungo hutegemea mahusiano ya kijamii yanayorejelewa na maneno fulani. Maneno hayo hupata maana kamili yanapotumiwa na wahusika kuhusiana katika tukio la mawasiliano. Kwa hivyo maneno hayo huweza kuonyesha vyeo, hadhi n.k.

Aidha suala la heshima huzingatiwa kwa kiwango kikubwa katika usonde jamii. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa usonde jamii husaidia watumizi wa lugha kuwasiliana kwa njia ya heshima.

Kunavyo vigezo vinne ambavyo hutumiwa kuonyesha heshima kati ya wahusika katika matamko, haya ni kwa mujibu wa Levinson (1979) ambaye aligawanya vipengele vyatjamii katika makundi mawili: kundi la mahusiano na kundi huru (halisi).

Tumetumia jedwali lifuatalo kutoa muhtasari wa kundi la mahusiano na kigezo cha heshima:

Jedwali 6: Vigezo vya Heshima

Aina ya Mahusiano	Kigezo cha Heshima
Msemaji na mrejelewa	Heshima kwa mrejelewa
Msemaji na msemewa	Heshima kwa msemewa
Msemaji na mtazamaji (ambaye si msemewa)	Heshima kwa mtazamaji (ambaye si msemewa)
Msemaji na muktadha	Viwango vya urasmi

Katika mahusiano ya msemaji na mrejelewa msemaji huonyesha heshima kwa mrejelewa. Mrejelewa au kirejelewa ni kile ambacho kinazungumziwa katika tamko. Msemaji huonyesha hadhi au cheo cha mrejelewa. Katika lugha ya Kiswahili kutaja vyeo vya warejelewa kama vile “bibi” badala ya “mwanamume” au “bwana” badala ya “mwanamume” huonyesha heshima kwa mrejelewa pamoja na hadhi yake. Mfano ufuatao unatutolea ufanuzi zaidi:

(57) (a) Yule *mwanamume* ameshindwa kuimba.

(b) Yule *bwana* ameshindwa kuimba.

Neno “mwanamume” kwenye (57a) linaweza kuzua dhana ya udhalilishaji kwa mrejelewa. Pia linaweza kuonyesha kuwa msemaji hamjui au hana uhusiano wa karibu na mrejelewa. Lakini kwa kutumia “bwana” (57b) msemaji anamwonyesha heshima mrejelewa hata kama hamjui (kwa sababu neno hili linazua dhana ya upole). Vivyo hivyo neno hilo pia linaweza kutaonyesha hadhi ya mrejelewa kuwa yeye ni tajiri au bingwa katika jambo fulani. Pia huenda amelitumia

neno hilo kwa njia ya kejeli kwa kutaka kukejeli tabia fulani za mrejelewa labda mrejelewa ni mtu mwenye kiburi. Mifano mingine ni kama vile:

(58) Alikuja kwenye *kasri* yangu.

(59) Kwetu ni *mbinguni*.

“Kasri” na “mbinguni” ni maneno yanayotaja kirejelewa. Katika (58) msemaji anaifananisha nyumba yake na kasri huku katika (59) msemaji anataka kuonyesha utakatifu wa nyumba yao.

Msemaji huonyesha heshima na hadhi kwa msemewa katika mahusiano ya msemaji na msemewa. Msemewa ni yule anayeambiwa tamko fulani kwenye tukio la mawasiliano. Kwa mfano:

(60) (a) *Mwalimu* nitaleta kitabu kesho.

(b) *Bi. Bhoke* nitaleta kitabu kesho.

Tutaangalia ufasiri wa matamko haya kwa namna mbili. Ikiwa ni mwanafunzi anayezungumza na mwalimu wake katika (60a) atakuwa ameonyesha heshima kwa mwalimu huyo kwa kutotaja jina lake mahususi. Kwenye tamko (60b) mwanafunzi huyo atachukuliwa kuwa amemkosea heshima mwalimu huyo wake. Hata hivyo ikiwa atakuwa anazungumza na mtu mwagine kumhusu mwalimu (ambapo mwalimu ni mrejelewa) anaweza kutaja jina lake mwalimu huyo. Kwa kutotaja jina la mwalimu na kutaja cheo chake mwanafunzi atakuwa ameonyesha kuwa mwalimu ana cheo cha juu kumliko yeye.

Ikiwa ni mwalimu kwa mwalimu mwenzake tamko (60a) litaonyesha mahusiano ya karibu, au mahusiano yasiyo rasmi. Lakini tamko (60b) litaonyesha urasmi wa mazungumzo hayo, pia kuwa msemaji ana cheo cha chini na msemewa ana cheo cha juu au pia kuonyesha kuwa hakuna uhusiano wa karibu kati ya msemaji na msemewa. Mifano mingine ni kama vile:

(61) *Bi. Mkubwa* mtoto amelala.

(62) Mshtakiwa ana kesi ya kujibu *mhesimiwa*.

Yaya anaonyesha heshima kwa mwajiri wake kwa kutaja cheo chake anapomrejelea (61) hali hii pia imejitokeza katika (62) ambapo wakili anataja cheo cha hakimu kwa kumrejelea.

Kigezo cha heshima katika mahusiano ya msemewa na mtazamaji huwa ni mtazamaji. Mtazamaji hapa si msemewa wala mrejelewa. Yeye ni yule ambaye kutokana na kuweko kwake karibu na msemewa au kuweko wakati wa matamko fulani, ambayo hayakuelekezwa kwake, ataweza kuyasikia matamko hayo. Kwa mfano mume anapozungumza na mkewe itambidi asitumie maneno fulani ambayo yanachukuliwa kuwa ni ya mwiko karibu na mama mkwe wake. Kwa kutotaja maneno hayo atakuwa ameonyesha heshima kwa mama mkwe.

Katika mahusiano ya msemaji na muktadha msemewa huonyesha hali mbalimbali na mazingira ambamo mazungumzo yanatokea. Kwa mfano katika muktadha rasmi matamko yatakuwa rasmi tofauti na muktadha usio rasmi. Kwa mfano:

- (63) (a) *Bwana Onyango* alinituma ofisini.
 (b) *Onyango* alinituma ofisini.

Tamko (63a) liko katika muktadha rasmi kwa sababu ya kutajwa kwa cheo “bwana”. Ikiwa mwanafunzi ndiye msemaji huenda anazungumza na mwalimu kuhusu mwalimu mwingine. Lakini ikiwa anazungumza na mwanafunzi mwenzake katika muktadha usio rasmi atatamka (63b).

Kundi la pili la vipengele vya jamii ni kundi huru (halisi). Levinson (1979) anaeleza kuwa kundi hili lina maneno ambayo yametengewa aina mbili mahususi za wahusika katika tukio la mawasiliano: msemaji idhinishwa na msemewa idhinishwa.

Kundi la msemaji idhinishwa linahusu maneno ambayo yametengewa watu fulani katika jamii kuyatamka. Kwa mfano kunaweza kuwa na maneno katika lugha ambayo yatatamkwa na wanawake pekee na yale ambayo yatatamkwa na wanaume pekee katika jamii husika. Neno “bee” ambalo ni la kuitikia wito limetengewa wanawake pekee katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo wanawake katika muktadha huu ndio wasemaji idhinishwa. Marmaridou (2000) anaeleza kuwa msemaji katika tamko akijirejelea kwa kutaja cheo chake atakuwa msemaji idhinishwa. Kwa mfano:

(64) (a) Mimi, *rais*, ninawahakikishia usalama wenu. (rais kwa wananchi)

(b) Mimi ninawahakikishia usalama wenu. (labda ni chifu kwa wanakijiji)

Msemaji wa (64a) ni rais ambaye anazungumza na wananchi tofauti na msemaji wa (64b) ambaye hana cheo cha urais. Rais ni msemaji idhinishwa kwa sababu ni yeye tu ana idhini (amekubaliwa) ya kujirejelea kama rais hii ni kutokana na hali halisi ya yeye kuwa rais. Msemaji wa (64b) si rais kwa hivyo hana idhini ya kujirejelea kwa kutumia jina rais.

Hadhira idhinishwa huonyeshwa na majina ya vyeo k.v. bwana, bi. mkubwa, mheshimiwa n.k. Katika kundi hili walioidhinishwa ni wahusika ambao si wasemaji katika tukio la mawasiliano. Hadhira inaweza kuwa msemewa au mrejelewa. Kwa mfano:

(65) (a) *Rais Museveni atakuja Kenya.* (Museveni ni mrejelewa ambaye ni rais wa nchi. Yeye ni msemewa idhinishwa kwa sababu ya cheo chake cha urais: anastahili kuitwa rais)

(b) “*Mheshimiwa Chelule, wanaeneo bunge lako wangependa kukutana nawe.*” (Chelule ni mheshimiwa kwa sababu ya kuwa mbunge kwa hivyo yeye ni msemewa idhinishwa: anastahili kuitwa kwa jina mheshimiwa)

Usonde jamii kama usonde nafsi hushirikisha matumizi ya kauli za mneni (Levinson, 1983). Zwicky (1974) kwa mujibu wa Marmaridou (2000) anaeleza kuwa kauli za mneni zina vipengele vya kijamii kwa sababu zinaonyesha mahusiano ya moja kwa moja kati ya msemewa na msemaji. Kwa mfano:

(66) *Bibi, nitakuona kesho.*

(67) “*Kutokana na ushahidi, baradhuli wewe, una kesi ya kujibu.*”

“Bibi” ni jina la kumrejelea mwanamke na ni mwito katika tamko (66). Neno hilo linaonyesha mahusiano rasmi kati ya msemaji na msemewa, pia kuwa msemaji na msemewa hawana uhusiano wa karibu, au linaweza kuonyesha mahusiano ya mwajiri (msemewa) na mwajiriwa (msemaji). “Baradhuli” ni tusi. Limetumiwa hapa kuonyesha kuwa hakuna mahusiano yoyote ya karibu kati ya msemewa na msemaji yaani hakuna urafiki baina yao.

Nafsi ya tatu pia huweza kutumiwa kuonyesha kipengele cha jamii katika usonde nafsi. Hata hivyo katika lugha ya Kiswahili hali hii haijitokezi iwapo viwakilishi nya nafsi ya tatu vitatumika katika tamko. Kwa mfano:

- (68) *Wao watakuja kesho asubuhi.*

Wao haionyeshi kigezo chochote cha jamii katika tamko hili. Hali hii ni tofauti katika tamko lifuatalo:

- (69) *Malkia atamrithisha mwanawe pesa nyingi.*

“Malkia” ni mrejelewa kwa hivyo katika tamko hili yeche ni nafsi ya tatu. Anatuonyesha tabaka la kijamii katika muktadha wa familia.

Fillmore (1971) anaeleza kuwa matumizi ya majina ya jamii ama pamoja na vimilikishi au kuyatumia pekee hutegemea mahusiano baina ya wahusika katika tukio la mawasiliano. Hali hii imejitokeza katika mifano yetu (51), (52), (53) na (54) ya awali.

3.4 HITIMISHO

Sura hii imejadili kwa kina kategoria mbili za usonde: usonde jamii na usonde nafsi. Tumeangazia namna ambavyo katika lugha ya Kiswahili viwakilishi nafsi, virejeshi na vimilikishi hutumika kuonyesha maneno ya usonde. Nafsi inapotumika kama kauli ya mneni huwa na mtagusano na vipengele nya kijamii. Hata hivyo suala hili la mtagusano baina ya kategoria hizi mbili za usonde, katika lugha ya Kiswahili, limebainika kwa baadhi ya matumizi ya nafsi ya pili na nafsi ya tatu hasa kwa kutumia majina wala sio viwakilishi nya nafsi ya tatu.

Sura hii imetuwekea msingi wa kuchanganua maneno ya usonde nafsi na usonde jamii katika lugha ya Kiswahili baina ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili.

SURA YA NNE
UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.1 UTANGULIZI

Data imegawanywa katika aina mbili za usonde: nafsi na jamii. Data hiyo imechanganuliwa kwa msingi wa uhusiano kwa kutumia utaratibu wa kusimba viwakilishi na utaratibu wa ufahamu katika nadharia ya uhusiano. Data ilikusanywa katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili darasani. Data yenyewe imenaswa kwenye santuri kama hifadhi.

4.2 USONDE NAFSI

Usonde nafsi huchunguza majukumu ya wahusika katika tukio la mawasiliano (Marmaridou, 2000). Majukumu haya huwa ya msemaji, msemewa na mrejelewa. Data ifuatayo katika sehemu hii inaonyesha majukumu haya.

4.2.1 Nafsi ya Kwanza

Nafsi ya kwanza katika umoja huashiria msemaji wa tamko kama inavyojitokeza katika matamko yafuatayo:

- (70) (a) *Nitaangalia karatasi ya kwanza, pili na tatu.*
 (b) *X: Nilisema unione asubuhi.*
 Y: Nilikuja lakini hukuwa afisini.
 (c) *Sijui kama nitapata nafasi ya kusahihisha vitabu vyenu.*
 (d) *Nitasahihisha vitabu kesho.*
 (e) *Niliwaambia kuwa kuna tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.*

“Ni” ni kiambishi cha nafsi ya kwanza katika umoja. Kiambishi hiki kinamrejelea msemaji katika tamko (70a-e).

Utaratibu wa kusimba viwakilishi “Mimi/Ni” ni: *kutambua kirejelewa kwanza kwa kumtambua msemaji*. Msemaji ni mwalimu katika (70a, b:X, c na d) kwa hivyo kirejelewa ni mwalimu.

Katika tamko (70b) “Y” ambaye ni msemaji, ni mwanafunzi: yeye ndiye anayerejelewa na kiwakilishi “ni”.

Aidha katika (70b) “X” na “Y” ni wasemaji na kwa upande mwingine “X” ni msemewa wa “Y” na “Y” akawa msemewa wa “X”. Tukio hili la mawasiliano linadhihirisha dhana ya kubadilisha majukumu ya wahusika katika tukio la mawasiliano ambapo kiini cha usonde kinabadilika kutoka kwa “X” hadi kwa “Y”.

Hatua zifuatazo za uzulishaji zilipitia akilini mwa wasemewa (mwalimu na wanafunzi) katika kumtambua mrejelewa wa kiambishi “ni”:

- i. Matamko haya yana maumbo ya kimantiki.
- ii. Kutokana na udhaniaji wa uhusiano, matamko haya yana uhusiano unaofaa zaidi.
- iii. Kiwakilishi “ni” kinapata uhusiano fulani kwa kuwa kimeashiria mtu/watu wanaojitokeza wazi katika miktadha hiyo ya matamko.
- iv. Mtu anayeashiriwa na “ni” katika (70a, b:X, c – e) ni msemaji ambaye ni mwalimu huku mwanafunzi akiwa msemaji katika (70b:Y).
- v. Dhana binafsi ya mwalimu na mwanafunzi inafikiwa kwa sababu hizo ndizo dhana zinazopatikana kwa urahisi katika miktadha hiyo ya matamko. Kupatikana kwa dhana hizo kumetumia jitahada ndogo na kutoa athari za kifahamu zinazofaa hatimaye kiwango tarajiwu cha uhusiano kinafikiwa.
- vi. Kinachoashiriwa na “ni” ni wasemaji ambao ni mwalimu na mwanafunzi katika umbo la kipropozisheni.

Kwa hivyo akilini mwa msemewa ufasiri wa “ni” kwa mfano, katika 70a utakuwa: Mwalimu ataangalia karatasi ya kwanza, pili na tatu huku katika 70b ufasiri wa “X” utakuwa mwanafunzi alikuja lakini hakunipata.

Nafsi ya kwanza wingi huonyeshwa kwa viwakilishi “sisi/tu”. Matumizi haya ya nafsi ya kwanza hayaonyeshi wazungumzaji wengi kwa pamoja kwa wakati mmoja; mzungumzaji huwa mmoja. Matamko yafuatayo katika (71-74) yanaonyesha matumizi mbalimbali ya nafsi ya kwanza wingi.

- (71) (a) *Ningependa tuangalie ufanuzi wa sentensi sahili.*
 (b) *Tulianza na kueleza fasihi ni nini.*
 (c) *Nilisema kuwa tutapitia aina za nomino tena.*
 (d) *Lazima tuanzie pale tujuapo hadi pale tusipojua.*
 (e) *Jana tulijadiliana kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi katika jamii.*
 (f) *Leo tujadiliane kuhusu tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.*

Kiambaishi “Tu” katika (71a-71f) kinamrejelea msemaji pamoja na wasemewa wake. Yaani wote, msemaji na wasemewa, wanahusika katika vitendo viliviyotajwa kwenye matamko hayo k.v. kuangalia, kueleza, kupitia, kujadiliana n.k.

Kutokana na utaratibu wa kusimba viwakilishi “Sisi/Tu” ambao ni: *kwanza tambua msemaji kisha tafuta kundi ambalo linarejelewa na msemaji*, msemaji ni mwalimu na kundi rejelewa ni mwalimu mwenyewe na wasemewa ambao ni wanafunzi.

Hatua mbalimbali za uzulishaji zilipitia akilini mwa wasemewa katika kufasiri kiwakilishi “tu”. Hatua zenyewe ni kama zile tulizoorodhesha katika (70). Tofauti ni kuwa kiwakilishi “tu” kinapata uhusiano fulani kwa kuwa kimeashiria mtu/watu wanaojitokeza wazi katika miktadha hiyo ya matamko. Wanaojitokeza wazi ni mwalimu na wanafunzi. Kwa hivyo akilini mwa wasemewa “tu” linaashiria mwalimu na wanafunzi kama kundi rejelewa.

- (72) (a) *Tuandike kuwa kundi nomino ni sehemu ya sentensi inayotoa taarifa kuhusu nomino.*
 (b) *Tukumbuke kubeba vitabu vya fasihi kesho.*

(c) *Tukifika kidato cha nne tutaangalia aina mbalimbali za virai tena.*

(d) *Hapo awali tuliandika kuwa tanzu ni nini?*

(e) *Leo tujikumbushe kuhusu tanzu za fasihi simulizi.*

(f) *Tunazijua insha za kiuamilifu?*

(g) *Ni lazima tuijandae vizuri katika mtihani huu.*

(h) *Tujifahamishe kuhusu mikondo ya maswali ya karatasi ya kwanza katika mitihani iliyopita.*

Matumizi ya “tu” katika matamko (72a-72h) yanaonyesha uhusika ambao msemaji hajashirikishwa kwenye kundi la warejelewa: warejelewa ni wasemewa pekee.

Katika kusimba viwakilishi “tu” msemewa kwanza atambua msemaji kisha atafuta kundi ambalo linarejelewa na msemaji. Kwa hivyo msemaji ni mwalimu na kundi rejelewa ni wanafunzi. Wanafunzi (kwa mfano) ndio wanaokumbushwa kuhusu tanzu za fasihi simulizi, wanaoenda katika kidato cha nne, wanaokumbushwa kubeba vitabu na wanaojiandaa kwa mtihani wala sio mwalimu.

Katika hatua za uzulishaji wa mrejelewa akilini mwa msemewa, kiwakilishi “tu” kinapata uhusiano fulani kwa kuwa linaashiria kundi linalojitokeza wazi katika miktadha hiyo ya matamko. Kundi hilo ni wanafunzi. Kwa hivyo akilini mwa wasemewa “tu” ni wanafunzi. Kwa mfano tamko (72e) litachukua umbo lifuatalo akilini mwa msemewa “leo wanafunzi wajikumbushe kuhusu tanzu za fasihi simulizi” huku (72g) likiwa “ni lazima wanafunzi wajijandae vizuri katika mtihani huu”.

Matumizi haya ya nafsi ya kwanza wingi hudhihirisha mahusiano ya kijamii kwa kuwa yana nia ya kuondoa mpaka wa kitabaka kati ya msemaji na msemewa. Mwalimu anapotumia nasfi hii kwa njia hii analeta uhusiano wa karibu kati yake na wanafunzi wake kwa kuijweka katika kiwango sawa nao.

Aidha matumizi ya nafsi ya pili wakati mwingine hayamshirikishi msemewa katika uhusika wake lakini humshirikisha “mwingine” (si msemaji wala msemewa) kama ifuatavyo:

- (73) (a) *Tulikuwa tukikusubiri darasani.*
- (b) *Mwalimu turuhusu tulete vitabu vyetu kesho.*
- (c) *Tumezungumza na walimu wengine na tukaamua kuja kusikiliza malalamishi yenu.*
- (d) *Sisi ni washirikishi katika mkutano huu.*
- (e) *Tumekuja hapa ili tuweze kuwasiliana nanyi kuhusu mtihani wa kitaifa.*

Katika kufasiri kiwakilishi “tu” msemewa kwanza atamtambua msemaji ambaye katika (73a na 73b) ni mwalimu na katika (73c-73e) ni wanafunzi. Baada ya kumtambua msemaji, msemewa hutafuta kundi ambalo linarejelewa na kiwakilishi hicho. Kundi rejelewa katika (73a na 73b) ni mwanafunzi na wanafunzi wenzake na katika (73c - 73e) ni mwalimu na walimu wenzake. “Wanafunzi wenzake” na “walimu wenzake” wanadhihirisha uhusika wa mwingine katika nafsi ya kwanza wingi: wao si wasemaji wala wasemewa.

Akilini mwa mwalimu (msemewa) katika (73a na 73b) kiwakilishi “tu” kinafikia kiwango tarajiwa cha uhusiano kwa kuashiria mwanafunzi na wanafunzi wenzake. Kwa hivyo umbo la kipropozisheni la tamko (73b), kwa mfano, litakuwa “mwanafunzi huyu na wanafunzi wengine wamekuwa wakinisubiri darasani”.

Hali hii pia itajitokeza katika akili ya msemewa (wanafunzi) katika tamko (73c - 73e). Yaani, kirejelewa cha “tu” ni mwalimu na walimu wenzake. Hivyo basi umbo la kipropozisheni la tamko (73d), kwa mfano, litakuwa “mwalimu huyu na walimu wenzake ni washirikishi katika mkutano huu”.

Uhusika katika nafsi ya kwanza wingi huweza kumshirikisha msemaji pekee kama ifuatavyo:

- (74) (a) *Kwa hivyo tunasema kuwa virai ni fungu la maneno katika sentensi ambalo halitoi maana kamilifu.*
- (b) *Tunachoeleza hapa ni kuwa shamirisho huwa mtendewa, mtendwa na kitumizi.*

Kiambishi “tu” katika “tunasema” na “tunachoeleza” kinamrejelea msemaji ambaye ni mwalimu. Kiambishi hiki hakijamshirikisha wanafunzi ambaye ni msemewa katika uhusika wake. Mwalimu ndiye anayetoa maelezo kuhusu virai na shamirisho katika matamko haya: hatoi maelezo hayo na wanafunzi.

4.2.2 Nafsi ya Pili

Nafsi ya pili humrejelea msemewa katika tukio la mawasiliano kama ifuatavyo:

- (75) (a) *Mbona mmechelewa kufika darasani?*
 (b) *Mkilipa karo mnapewa risiti.*
 (c) *Mnazijua tofauti hizo?*
 (d) *Unataka kuonyesha kuwa umebobea katika Kiswahili.*
 (e) *X: Ulikuja asubuhi kweli?*

Y: Ndiyo, nilikuja ulivyonieleza.

“M” na “u” ni viambishi vya nafsi ya pili wingi. Msemaji ni mwalimu katika (75a – 75e:X) na wanafunzi katika (75e:Y).

Utaratibu wa kusimba viwakilishi “Nyinyi/M” na “Wewe/U” ni: *kutambua mrejelewa kwanza kwa kutambua msemewa*. Wasemewa ni wanafunzi kwa hivyo warejelewa ni wanafunzi wao hao katika (75a – 75e:X). Mwalimu ni msemewa na ndiye mrejelewa katika (75e:Y).

Katika (75e) dhana ya kiini cha usonde inajitokeza. Wahusika katika tukio hili la mawasiliano wanabadilishana majukumu ya kuwa msemaji na msemewa. “X” ni msemaji na “Y” ni msemewa wake. Kisha “Y” anachukua zamu ya kuwa msemaji na “X” kuwa msemewa wake. Kiini cha usonde kinabadilika kutoka kwa “X” hadi kwa “Y”.

Hatua zifuatazo za uzulishaji zilipitia akilini mwa wasemewa (mwalimu na wanafunzi) katika kumtambua mrejelewa wa kiambishi “u” na “m”:

- i. Matamko haya yana maumbo ya kimantiki
- ii. Kutokana na udhaniaji wa uhusiano, matamko haya yana uhusiano unaofaa zaidi.
- iii. Viwakilishi “m” na “u” vinapata uhusiano fulani kwa kuwa vimeashiria mtu/watu wanaojitokeza wazi katika miktadha hiyo ya matamko.
- iv. Mtu anayeashiriwa na “m” na “u” katika ni wasemewa ambao ni wanafunzi na mwalimu.
- v. Dhana binafsi ya mwalimu na wanafunzi inafikiwa kwa sababu hizo ndizo dhana zinazopatikana kwa urahisi katika miktadha hiyo ya matamko. Kupatikana kwa dhana hizo kumetumia jitahada ndogo na kutoa athari za kifahamu zinazofaa hatimaye kiwango tarajiwa cha uhusiano kinafikiwa.
- vi. Kinachoashiriwa na “m” na “u” ni wasemewa ambao ni wanafunzi na mwalimu katika umbo la kipropozisheni.

Matumizi ya nafsi ya pili huonyesha matamko yenyе maagizo ambayo katika muktadha huu wa mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi mrejelewa hubainika wazi kuwa ni mwanafunzi. Matamko yafuatayo yanabainisha hali hii:

- (76) (a) *Uifanye insha yako imvutie mtahini.*
 (b) *Ukiandika insha yako onyesha uwezo wako wa kuwasiliana.*
 (c) *Mtaandika kuhusu kauli ya kutendeana na kutendana.*
 (d) *Unapotofautisha tumia maneno kama: ilhali, huku na ingawa.*

Wasemewa katika (76) ni wanafunzi na wanafunzi hao ndio warejelewa wa viambishi “m” na “u”. Mwalimu ambaye ni msemaji anawapatia wanafunzi maagizo.

Mwalimu huyu anatumia nafsi ya pili umoja hata anapozungumza na wanafunzi wengi. Matumizi ya umoja yanababisha athari kwa ufahamu wa mwanafunzi: yaani mwanafunzi atajitambulisha na maagizo hayo (maagizo yanamlenga yeye mwenyewe). Kwa hivyo akilini mwake kinachoashiriwa na “u” sio wanafunzi lakini ni yeye binafsi. Kwa mfano, ufasiri wa (76a) utakuwa, “mimi niifanye insha yangu imvutie matahini” na (76b) kuwa, “mimi nikiandika

insha yangu nionyeshe uwezo wangu wa kuwasiliana". Kiambishi "U" kinapofikia kiwango hicho vha uhusiano katika uzulishaji wa msemewa basi mwalimu atakuwa amefaulu katika lengo ujumbe wake.

Matumizi ya nafsi ya pili yamedhihirisha mahusiano kati ya msemaji na msemewa. Nafasi ya mwalimu katika muktadha huu ni kuwa ana idhini ya kuwapa wanafunzi maagizo lakini wanafunzi hawawezi kumpatia maagizo.

4.2.2.1 Kauli za Mneni

Nafsi ya pili hubainisha matumizi ya kauli za mneni katika matamko kama ifuatavyo:

- (77) (a) *Nyinyi, mbona hamkumaliza kazi zenu?*
 (b) *Wewe, Opiyo⁹ acha kutudanganya.*
 (c) *Wewe msichana ingia na iwe mara ya mwisho.*
 (d) *Nyinyi, nyamazeni!*
 (e) *We! Fuata maagizo uliyopewa ukifanya kazi hii.*
 (f) *Nendeni uwanjani nyinyi.*
 (g) *Soma wewe.*

Katika matamko (77a – 77e) viwakilishi vya nafsi vimetumiwa kuonyesha mwito huku visemewa vikibainika katika matamko (77f – 77g).

Msemaji katika matamko haya ni mwalimu. Wasemewa ni wanafunzi ambao ndio wanaorejelewa na viwakilishi "wewe", "nyinyi" na "we."¹⁰

⁹ Majina yote yamebadilishwa.

¹⁰ Ufupisho wa nafsi ya pili huru "wewe"

Matumizi ya nafsi ya pili katika kauli za mneni hudhihirisha mahusiano kati ya msemaji na msemewa: mahusiano kati ya mwalimu na wanafunzi. Katika mahusiano hayo, kwa mfano, mwalimu huweza kutoa onyo (77c), kuamrishwa wanafunzi (77d – 77g), kuonyesha dhihaka (77a na 77c) au kuonyesha msisitizo wa anayezungumziwa.

4.2.3 Nafsi ya Tatu

Nafsi ya tatu huonyeshwa kwa viwakilishi “yeye/a” na “wao/wa” katika umoja na wingi mtawalia kama ifuatavyo:

- (78) (a) *Alizungumzia yale ambayo tumeyasema hapa darasani.*

(b) *Akija mwambieni aje anione.*

(c) *Wameanza kuleta vipengele vingine tofauti kabisa.*

(d) *Anasinzia darasani kila mara.*

(e) *Alituambia tuchukue vitabu kesho.*

(f) *Amefungia kitabu changu kwenye dawati lake.*

Msemaji katika (78a – 78c) ni mwalimu huku mwanafunzi akiwa msemaji katika (78d – 78f).

Utaratibu wa kusimba viwakilishi “yeye/a” na “wao/wa” ni: *kutambua dhana binafsi yenyeye sifa ya “yeye/a” na “wao/wa”* katika miktadha ya matamko hayo. Kwa hivyo:

- i. Kiambishi “a” katika (78a) kinamrejelea mwalimu lakini mwalimu huyo ni tofauti na mwalimu ambaye anazungumza. Mwalimu huyo mrejelewa yupo kwenye mahala na wakati wa kusemwa kwa tamko hilo.
 - ii. Kiambishi “a” katika (78b) kinamrejelea mwanafunzi tofauti na wale ambao ni wasemewa.
 - iii. Kiambishi “wa” katika (78c) kinarejelea walimu ambao ni watahini katika mtihani wa kitaifa.

- iv. Kiambishi “a” katika (78d) kinamrejelea mwanafunzi ambaye hata kama yupo mahali na wakati wa kusemwa kwa tamko hilo, yeye si msemewa.
- v. Kiambishi “a” katika (78e) kinamrejelea mkutubi wa shule.
- vi. Kiambishi “a” katika (78f) kinamrejelea mwanafunzi tofauti na wasemewa: mwanafunzi huyo hayuko katika mahali na wakati wa kusemwa kwa tamko hilo.

Kinachobainika hapa ni kuwa nafsi ya tatu huonyesha kirejelewa (mrejelewa) katika tukio la mawasiliano. Mrejelewa huyu si msemewa wala msemaji.

Virejelewa, kwa mfano, mkutubi, walimu watahini na mwanafunzi anayesinzia ni dhana binafsi zeny sifa za “a” na “wa”. Akilini mwa wasemewa viambishi “a” na “wa” vinapata uhusiano wa aina fulani kwa kuashiria dhana binafsi inayojitokeza wazi katika miktadha hiyo ya matamshi. Kwa hivyo ufasiri wa “a” na “wa” unafikia kiwango tarajiwa cha uhusiano akilini mwa msemewa wakati ambapo virejelewa vyao vimebainika. Kwa mfano, umbo la kipropozisheni la tamko (78e) akilini mwa msemewa litakuwa, “mkutubi alimwaambia mwanafunzi huyu na wanafunzi wengine wachukue vitabu kesho”.

4.2.4 Vimilikishi

Vimilikishi huonyesha kuwa kitu fulani kinamilikiwa na mtu fulani. Vimilikishi hivi, tulivyoeleza awali, huundwa kwa mofimu {-angu}, {-etu}, {-ako}, {-enu}, {-ake} na {-ao} kutegemea nafsi pamoja na upatanisho wa kisarufi wa ngeli. Ikumbukwe ya kuwa “yangu” ya msemaji, kwa mfano, ni tofauti na “yako” ya mtu wa pili au “yake” ya mtu wa tatu. Vimilikishi hudhihirika ifuatavyo katika matamko:

- (79) (a) *Amefungia kitabu changu kwenye dawati lake.*
- (b) *Mwalimu wako anakuita.*
- (c) *Nyinyi, mbona hamkumaliza kazi zenu?*
- (d) *Ukiandika insha yako onyesha uwezo wako wa kuwasiliana.*

Katika (79) “changu”, “wako”, “yako”, “zenu” na “lake”, ni vimilikishi. Wasemaji katika matamko haya wanadhihirika ifuatavyo: katika (79a na 79b) mwanafunzi ndiye msemaji huku mwalimu akiwa msemaji katika (79c na 79d).

“Changu” (79a) ni kimilikishi cha nafsi ya kwanza umoja na kinarejelea kitabu cha msemaji ambaye ni mwanafunzi. Msemewa ni mwalimu huku kiambishi “a” kinaashiria mwanafunzi ambaye alikifungia kitabu. Kitabu cha msemaji sicho kile cha mwanafunzi huo mwingine. Vivyo hivyo “lake” linarejelea dawati la mwanafunzi huyo mwingine wala si la msemaji.

“Wako” (79b) ni kimilikishi cha nafsi ya pili umoja na kinarejelea mwalimu wa msemewa: msemewa ni mwanafunzi. Matumizi haya yanaonyesha kuwa mwalimu wa msemaji siye mwalimu wa msemewa. Matumizi haya pia yanaweza kuonyesha kuwa msemewa ana mwalimu ambaye ana uhusiano wa karibu naye kuliko wanafunzi wengine.

“Zenu” (79c) ni kimilikishi cha nafsi ya pili wingi na kinarejelea kazi ya wasemewa: wasemewa ni kundi fulani la wanafunzi. Matumizi haya yanaonyesha kuwa kazi za wanafunzi hawa zinatofautiana kutoka mwanafunzi mmoja hadi mwingine katika kundi hilo.

“Yako” na “wako” (79d) ni vimilikishoi vya nafsi ya pili umoja na vinarejelea insha na uwezo wa wasemewa: wasemewa ni wanafunzi (taz. 76 uk. 52). Matumizi haya yanaonyesha kuwa kila mwanafunzi huandika insha na insha ya mwanafunzi mmoja haifanani na ya mwanafunzi mwingine. Vivyo hivyo uwezo wa kuwasiliana huwa tofauti kutoka mwanafunzi mmoja hadi mwingine.

Katika hatua za uzulishaji wa mrejelewa akilini mwa msemewa, kimilikishi “changu”, kwa mfano, kinapata uhusiano fulani kwa kuwa kinaashiria dhana inayojitokeza wazi katika muktadha wa tamko (79a). Dhana hiyo ni kitabu cha msemaji. Kwa hivyo akilini mwa msemewa, tamko hilo litachukua umbo lifuatalo la kipropozisheni: “mwanafunzi mwingine amefungia kitabu cha msemaji (mwanafunzi huyu) kwenye dawati lake”.

Matumizi ya baadhi ya vimilikishi huweza kudhihirisha mahusiano baina ya wahusika kwenye tukio la mawasiliano ilivyobainika katika matumizi ya “wako” kwenye tamko (79b).

4.3 USONDE JAMII

Usonde jamii huhusu kutambua mahusiano ya kijamii baina ya wahusika katika tukio la mawasiliano. Maana ya tungo hutegemea mahusiano ya kijamii yanayorejelewa na maneno fulani. Maneno hayo hupata maana kamili yanapotumiwa na wahusika kuhusiana katika tukio la mawasiliano.

Suala la heshima huangaziwa kwenye mahusiano ya wahusika katika tukio la mawasiliano. Kwa mfano:

- (80) (a) *Mwalimu, nitaleta kitabu kesho.*
 (b) *Bi. Onyango amenitura kuchukua kitabu chake.*
 (c) *Umemaliza kazi ya Awiti?*
 (d) *Omino, nenda ukamwone mwalimu mkuu.*

Maneno “mwalimu”, “bi.” na “mkuu” ni maneno ya usonde. Yametumiwa kutaja vyeo vyta wahusika warejelewa katika matamko haya.

Wasemaji ni mwanafunzi (80a – 80c) huku msemaji katika (80d) ni mwalimu. Wasemewa ni mwalimu (80a na 80b) na mwanafunzi (80c na 80d). Kigezo cha heshima katika matamko haya huwa ni mrejelewa: yaani msemaji huonyesha heshima kwa kirejelewa kwa kutaja vyeo vyake (katika muktadha ya mwalimu-mwanafunzi). Kwa hivyo, mwanafunzi kwenye (80a) anataja cheo “mwalimu” anapozungumza na mwalimu huyo kwa madhumuni ya kumwonyesha heshima.

Katika (80b) mwanafunzi anazungumza na mwalimu kuhusu mwalimu mwingine. Mwanafunzi huyo anaonyesha heshima kwa mwalimu huyo mrejelewa. Anafanya hivi kwa kutomtaja kwa jina lake mahususi pekee ila analitaja jina hilo kwa kulishirikisha na cheo “bi”.

Mwanafunzi anazungumza na mwanzo mwenzake katika (80c). Mrejelewa hapa ni mwalimu ambaye anaitwa “Awiti”. Ikiwa mwanafunzi huyu angekuwa akizungumza na mwalimu yuyo huyo au labda awe anazungumza na mwalimu mwingine ye yeyote atakuwa amekosa kumwonyesha heshima mwalimu mrejelewa.

Mwalimu kwa kutaja cheo “mwalimu mkuu” katika (80d) anapozungumza na mwanafunzi anaonyesha heshima kwa mwalimu mwingine mwenye cheo cha juu kuliko chake.

Msemewa, kwa mfano, katika tamko (80c) anapofanya uzulishaji wa kirejelewa anahusisha “Awiti” na mwalimu. Yaani neno “Awiti” linapata uhusiano kwa kuwa linaashiria dhana binafsi ya mtu anayejitokeza wazi na mwenye sifa ya “Awiti” katika muktadha wa tamko hilo. Kwa hivyo anayeashiriwa na “Awiti” ni mwalimu. Umbo la kipropozisheni la tamko hili litakuwa: “nimemaliza kazi ya mwalimu?”

Aidha katika usonde jamii muktadha pia huonyeshwa kwa kudhihirisha viwango vyta urasmi. Kwa mfano, katika (80a) (80b) na (80d) muktadha wa mawasiliano hayo ni rasmi tofauti na ule wa (80c) ambao si rasmi. Tunasema kuwa muktadha katika (80c) si rasmi kwa sababu mwanafunzi huyu ikiwa atazungumza na mwanafunzi mwenzake katika muktadha rasmi angelitaja jina la mwalimu mrejelewa kwa kutaja cheo bwana au mwalimu. Kwa hivyo angemrejelea mwalimu huyo kama “Bwana Awiti” au “mwalimu Awiti”.

Usonde jamii huonyesha idhini ya wahusika katika tukio la mawasiliano ya kutumia maneno fulani kujirejelea au kumrejelea msemewa: msemewa idhinishwa na msemaji idhinishwa. Kwa mfano:

(81) (a) *Sisi walimu tunataka muwe na matokeo mazuri.*

(b) *Omino, nenda ukamwone mwalimu mkuu.*

Neno “walimu” katika (81a) linabainisha kundi la msemaji idhinishwa. Mwalimu ambaye ndiye msemaji wa tamko hili anajirejelea pamoja na walimu wengine kwa kutaja cheo chao cha ualimu. Anazungumza na wanafunzi ambao si walimu kwa hivyo mwalimu ameidhinishwa kujirejelea kwa kutumia cheo chake.

Vivyo hivyo, neno “mwalimu mkuu” limetumika kubanisha kundi la mrejelewa idhinishwa. Mwalimu ambaye ni msemaji wa tamko hili anamrejelea mwalimu mwingine mwenye cheo cha juu kuzidi chake. Pamoja na cheo, mwalimu huyu anazungumza na mwanafunzi kwa hivyo kwa kutaja “mwalimu mkuu” anadhihirisha urasmi wa muktadha wa mazungumzo hayo.

Katika hatua za uzulishaji akilini mwa msemewa wa tamko (81b) kinachoashiriwa na “mwalimu mkuu” ni mtu mwenye cheo cha juu kumzidi mwalimu (msemaji). Umbo la kipropozisheni la tamko hili litakuwa : “mimi niende nikamwone mwalimu mwenye cheo cha juu zaidi”.

Hali hii pia inabainika katika (80a) ambapo mwalimu ni kundi la msemewa idhinishwa. Mwanafunzi anataja cheo chake cha ualimu anapozungumza naye.

Vimilikishi pia hutumiwa kubainisha matumizi ya usonde jamii katika matamko. Kwa kurejelea tamko (79b uk. 56) “wako” ni kimilishi cha nafsi ya pili umoja. Kinaweza kuwa kimetumiwa katika tamko hilo ili kuonyesha kuwa msemewa ana mwalimu ambaye ana uhusiano wa karibu naye kuliko wanafunzi wengine au kuwa mwalimu wa msemewa ni tofauti na mwalimu wa msemaji.

Kauli za mneni pia hutumiwa kuonyesha mahusiano baina ya wahusika katika tukio la mawasiliano kama ifuatavyo:

(82) *Mvulana, njoo nikutume.*

Neno “mvulana” ni mwito kwenye tamko (82). Tamko hili limesemwa na mwalimu kwa wanafunzi. Matumizi ya neno hilo yanaonyesha kuwa msemaji na msemewa hawana uhusiano wa karibu; yaani mwalimu hamjui wanafunzi huyo kwa jina lake.

Msemewa wa tamko hili ni wanafunzi kwa hivyo yeye ndiye mrejelewa wa neno mvulana. Katika uzulishaji wa kirejelewa msemewa anahusisha mvulana na yeye mwenyewe. Yaani neno mvulana linapata uhusiano kwa kuwa linaashiria dhana binafsi ya mtu anayejitokeza wazi na mwenye sifa ya “mvulana” katika muktadha wa tamko hilo. Anayeashiriwa na “mvulana” ni msemewa. Umbo la kipropozisheni la tamko hili kwa hivyo litakuwa: “mimi niende mwalimu anitume”.

Matamko (77a – 77g) pia yanabainisha matumizi ya kauli za mneni kuonyesha mahusiano baina ya wahusika katika tukio la mawasiliano.

4.4 MAJADILIANO

Utaratibu wa kusimba viwakilishi umetumiwa katika kueleza msemewa, mrejelewa na msemaji katika tamko. Pamoja na hayo tumetumia hatua za kufikia uzulishaji akilini mwa msemewa kama zilivyoorodheshwa na Sperber na Wilson (1995) kufikia kirejelewa katika maneno ya usonde.

Uchanganuzi huu umebainisha kuwa maneno ya usonde nafsi yanajitokeza katika nafsi ya kwanza, pili na ya tatu. Kwa kiwango kikubwa zaidi maneno ya usonde nafsi yanajitokeza katika nafsi ya kwanza wingi ambapo hali tatu za matumizi ya maneno hayo zimebainika ifuatavyo: matumizi ambapo msemewa hashirikishwi katika uhusika wa nafsi hiyo, msemewa na msemaji ni wahusika na hali ambapo msemaji si mhusika katika nafsi hiyo. Matumizi ya nafsi ya pili wingi yasiyomshirikisha msemaji katika uhusika yanaonyesha kipengele cha kijamii ya kwamba msemaji anatumia nafsi ya pili katika unenaji wake lakini kwa msingi wa kutaka kujitambulisha na msemewa wake. Yaani anaziba mipaka ya kihadhi iliyopo baina yao.

Dhana ya kiini cha usonde imedhihirishwa katika uchanganuzi huu wahusika hubadilisha majukumu yao ya kuwa msemaji na msemewa. Msemaji huwa msemewa na msemewa akawa msemaji.

Matumizi ya nafsi ya pili katika usonde humrejelea msemewa. Kilichobainika ni kuwa nafsi ya pili inapotumiwa kwenye kauli za mneni kipengele cha mahusiano ya kijamii kinaangaziwa. Mahusiano hapa ni ya mwalimu-mwanafunzi ambapo mwalimu kwa sababu ya nafasi yake ya kuwa katika hadhi ya juu anatumia ukali kwenye matamko yake kutoa amri na kuonya wanafunzi. Pamoja na hayo, nafsi ya pili imeonyesha kuwa katika mahusiano ya mwalimu-mwanafunzi mwalimu hutoa maagizo kwa wanafunzi (kutokana na nafasi yake kwenye mahusiano hayo).

Marmaridau (2000) ameshikilia kuwa nafsi ya tatu ni njia hafifu sana ya kuonyesha usonde anaongezea kuwa ili kuonyesha usonde katika nafsi hii majina mahususi ya warejelewa hutumiwa. Hata hivyo tumebainisha kuwa lugha ya Kiswahili ina viambishi maalumu vya kuonyesha nafsi ya tatu: “yeye/a” na “wao/wa”. Viwakilishi hivi ni vya usonde kwa sababu kutakuwa na haja ya kumjua anayerejelewa kama “a” na “wa” wakati wa kufasiri ujumbe wa

tamko hili. Wakati mwingine msemaji huweza kutumia kidole ama njia nyingine kuonyesha yule ambaye anamrejelea hivyo basi atakuwa amemshirikisha mtu huyo katika muktadha wa tamko.

Aidha katika usonde jamii suala la heshima linajitokeza. Heshima kulingana na data yetu huwa kwa mwalimu kutoka kwa mwanafunzi. Kauli za mneni na vimilikishi pia hutumiwa katika usonde jamii kuonyesha mahusiano baina ya msemewa na msemaji.

4.5 HITIMISHO

Sura hii imechanganua maneno ya usonde jamii na usonde nafsi kwa kutambua msemaji, msemewa na mrejelewa katika tukio la mawasiliano. Data ambayo imechanganuliwa ni matamshi katika mawasiliano ya walimu na wanafunzi ya Kiswahili. Data yenyewe ilikuwa jumla ya maneno 64. Tumebainisha namna ambavyo katika lugha ya Kiswahili viwakilishi nafsi, na vimilikishi hutumika kuonyesha maneno ya usonde. Nafsi inapotumika kama kauli ya mneni huwa na mtagusano na vipengele vya kijamii. Hata hivyo suala hili la mtagusano baina ya kategoria hizi mbili za usonde, katika lugha ya Kiswahili, limebainika kwa baadhi ya matumizi ya nafsi.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 UTANGULIZI

Baada ya kuchanganua matokeo ya utafiti katika sura iliyotangulia hii, hitimisho na mapendekozero yametolewa katika sura hii. Hitimisho limetolewa kwa msingi wa kutathmini malengo ya utafiti na nadharia tete zilizokuwa zikiongoza utafiti huu. Haya ni kwa mujibu wa kutatua tatizo la utafiti huu kuhusu uwiano wa usonde nafsi na usonde jamii.

5.2 HITIMISHO

Kutokana na malengo ya utafiti huu tumeweza kubainisha ya kuwa:

Mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahilli katika shule za upili huwa na maneno ya usonde nafsi.

Walimu na wanafunzi wa Kiswahili hutumia maneno ya usonde jamii katika mawasiliano yao.

Kategoria ya usonde nafsi na usonde jamii huwa na uhusiano lakini uhusiano huo haujitokezi katika matumizi yote ya usonde nafsi; ni katika baadhi ya matumizi ya usonde nafsi ndipo tupata vipengele vya kijamii vikijitokeza. Hali hii kwa hivyo ni tofauti na msimamo wa Marmaridau (2000) kuwa kuna uhusiano kati ya usonde nafsi na usonde jamii kwa kiasi ambacho kategoria moja haiwezi kutumiwa pasi na kuirejelea kategoria hiyo ingine.

Nadharia ya uhusiano ya Sperber na Wilson (1986/1995 na 1993) inatosheleza kuchanganua maneno ya usonde nafsi na usonde jamii. Utoshelezi huu unatokana na utaratibu wa kusimba viwakilishi pamoja na hatua za uzulishaji zinazotokea akilini mwa msemewa ili kufikia mrejelewa na maana lengwa katika tamko.

Kulikuwa na nadharia tete nne katika utafiti huu:

Tumebainisha kuwa mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahilli katika shule za upili huwa na maneno ya usonde nafsi.

Utafiti huu pia umebainisha kuwa mawasiliano ya walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili huwa na maneno ya usonde jamii.

Utafiti huu umebainisha kuwa uhusiano uliopo baina ya usonde nafsi na usonde jamii hutokea katika kauli za mneni na katika matumizi ya nafsi ya kwanza wingi ambapo msemaji hashirikishwi kwenye uhusika. Aidha kwa kutaja vyeo vya warejelewa, usonde jamii hudhihirishwa kwenye tamko.

Tumebainisha kuwa nadharia ya uhusiano inatosheleza katika uchanganuzi wa maneno ya usonde (usonde nafsi na usonde jamii).

5.3 MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto ya vitabu vya kurejelea matumizi ya usonde nafsi na usonde jamii katika lugha ya Kiswahili. Kazi nyingi tulizokutana nazo zimeshughulikia vionyeshi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo kuna haja ya kufanya utafiti kuhusu matumizi ya kategoria zote za kimsingi za usonde (usonde nafsi, usonde jamii, usonde mahali, usonde wakati na usonde diskosi) katika lugha ya Kiswahili sio tu kwenye shule za upili lakini katika viwango vingine vya elimu na katika nyanja nyinginezo za kijamii.

Utafiti huu ulijkita katika matumizi ya usonde nafsi na usonde jamii kwa msingi wa uhusiano. Kuna haja ya kutafitia suala la upole jinsi linavyojitokeza kwenye kategoria hizi mbili za usonde katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa madhumuni ya kutaka kubainisha ikiwa kwa kuzingatia kigezo cha upole kutakuwa na uhusiano sisisi kati ya kategoria hizi mbili za usonde kwa kiasi cha kuchukuliwa kama kategoria moja.

MAREJELEO

- Bataller, S.M. (2003/2004). *Lexical Pragmatics: Relevance Theory and Generalised Conversational Implicature*. Anglogermanica Online.
- Bühler, K. (1934). The Deictic Field of Language and Deictic Words. In Robert J. Jarvella & Wolfgang Klein (Eds.). *Speech, Place and Action: Studies in Deixis and Related Topic*, 9-30. Chichester, New York, Brisbane, Toronto & Singapore: John Wiley & Sons Limited.
- Carston, R. (2002). *Thoughts and Utterances: The Pragmatics of Explicit Communication*. Oxford: Blackwell.
- Fillmore, C. (1971). *Lectures on Deixis*. Berkley: University of Carlifonia.
- Firth, R.J. (1950). Personality and Language in Society. In *Papers in Linguistics*, 177-189 . Oxford: Oxford University Press.
- Grice, H.P. (1975). Logic and conversation. In: Cole, P. & Morgan, J. (eds.) *Syntax and Semantics 3: Speech Acts*, 41-58. New York: Academic Press
- Grundy, P. (2000). *Doing Pragmatics*. New York: Oxford University Press.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Huang, Y. (2000) *Anaphora: A Cross-linguistic Study*. Oxford: OUP.
- Ingram, D. (1971). Toward a Theory of person Deixis. *Papers in Linguistics* 4, 37-54.
- Kathori C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. (Second Revised Edition). Delhi: New Age International (P) Limited.
- Levinson, S. (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- _____. (1996). Frames of reference and Molyneux's question: Cross-linguistic evidence. In P. Bloom & M. Peterson & L. Nadel & M. Garrett (Eds.). *Language and space*. Cambridge, MA: MIT Press.

- Lyons, J. (1983). *Introduction to Theoretical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University
- Marmaridou, Sophia S.A. (2000). *Pragmatics Meaning and Cognition*. Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.
- Mukhwana, A. & Obuchi, S. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Nairobi: A-Frame Publishers.
- Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Mweri, G.J. (2010). *Utangulizi wa Isimu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Nicolle, S. (2007). Metarepresentational Demonstratives in Digo. In R. A. Nilsen, Amfo N. N. A, and Borthen K. (eds.). *Interpreting Utterances: Pragmatics and its Interfaces. Essays in Honour of Thorstein Fretheim*. Oslo: Novus.
- Otwere, S. (2012). Usonde Katika Tafsiri: Tathmini ya Mafundisho ya Biblia katika Shule ya Sabato kwa Watu Wazima. Tasnifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Powell, G. (1998). The Deferred Interpretation of Indexicals and Proper Names. *UCL Working Papers in Linguistics* 10.
- Renkema, J. (1993). *Discourse Studies: An Introductory Textbook*. Amsterdam: John Benjamin Publishing Company.
- Rubio-Fernandes, P. (2008). Concept Narrowing: The Role of Context Independent Information. *Journal of Semantics* (Electronic Version). Oxford University Press.
- Sperber, D. & Wilson, D. (1986/1995). *Relevance: Communication and Cognition*. Oxford: Blackwell.
- _____. (1993). Linguistic Form and Relevance. *Lingua* 90, 1-25.

- Sperber, D. & Wilson, D. (2002). Pragmatics, Modularity and Mind-reading. *Mind and Language* 17, 3-23.
- Wilson, D. & Carston, R. (2007). A Unitary Approach to Lexical Pragmatics: Relevance, Inference and Ad Hoc Concepts. In Burton-Roberts, N. (ed.). *Pragmatics*, 230-259. London: Palgrave,
- Yule, G. (1985). *The Study of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.
- _____. (1996). *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press. Online Resources.

KIAMBATANISHO

ISTILAHİ

Athari za jitihada	<i>Effort effects</i>	Mazingira ya fahamu	<i>Cognitive environment</i>
Athari za kifahamu	<i>Cognitive effects</i>	Mrejelewa	<i>Referent</i>
Data ya kimsingi	<i>Primary data</i>	Msemaji idhinishwa	<i>Authorised speaker</i>
Dhana binafsi	<i>Individual concept</i>	Msemewa idhinishwa	<i>Authorised addressee</i>
Gharama ya mchakato	<i>Processing cost</i>	Msemewa	<i>Addressee</i>
Jitihada za mchakato	<i>Processing effort</i>	Mtu anayejitokeza wazi kimuktadha	<i>Contextually salient individual</i>
Kanuni fahamu	<i>Cognitive principle</i>	Muktadha	<i>Context</i>
Kanuni mawasiliano	<i>Communicative principle</i>	Mwito	<i>Calls</i>
Kauli za mneni	<i>Vocatives</i>	Nadharia tete fasiriwa	<i>Interpretive hypothesis</i>
Kiashiria	<i>Stimulus</i>	Sampuli maksuudi	<i>Purposive sampling</i>
Kiashiria wazi	<i>Ostensive stimulus</i>	Simbwa	<i>Coded</i>
Kiini cha usonde	<i>Deictic centre</i>	Tamko	<i>Utterance</i>
Kiunzi husiano cha urejeleo	<i>Relative frame reference</i>	Tamko fiche	<i>Implicatures</i>
Kiunzi Kamili	<i>Absolute frame</i>	Tamko la kiisimu	<i>Linguistic utterance</i>
Kundi huru/halisi	<i>Absolute group</i>	Tamko wazi	<i>Explicatures</i>
Kuonyesha/ishara	<i>Pointing</i>	Taratibu zenyе vikwazo	<i>Procedural constraints</i>
Lengo mawasiliano	<i>Communicative intent</i>	Tukio la mawasiliano	<i>Speech event</i>
Lengo ujumbe	<i>Informative intent</i>	Ubanaji	<i>Narrowing</i>
Matumizi ya usonde	<i>Deictic usages</i>	Udhaniaji wa hali bora zaidi	<i>Presumption of optimal relevance</i>
Mawasiliano wazi	<i>Ostensive communication</i>		

Udhaniaji	<i>Presumption</i>
Uhusiano	<i>Relevance</i>
Uhusiano bora zaidi	<i>Optimal relevance</i>
Uhusiano pevu	<i>Maximal relevance</i>
Ukadiriaji	<i>Approximation</i>
Umbo la kipropozisheni	<i>Propositional form</i>
Umbo la kimantiki	<i>Logical form</i>
Upanuaji	<i>Broadening</i>
Usonde	<i>Deixis</i>
Usonde jamii	<i>Social deixis</i>
Usonde nafsi	<i>Person deixis</i>
Utafiti maelezo	<i>Descriptive research</i>
Utafiti stahilifu	<i>Qualitative research</i>
Utafiti wiano	<i>Comparative research</i>
Utaratibu wa kueleza viwakilishi	<i>Procedural pronoun encoding</i>
Utaratibu wa kusimba	<i>Procedural encoding</i>
Uzulishaji	<i>Inference</i>
Visemewa	<i>Addresses</i>
Vitendo usemi	<i>Speech acts</i>